**Waefeso**

Mtaala

## I. Habari kwa Ujumla

A. Mkufunzi: Don Walker na kutafsiriwa na Chris Mwakabanje

B. Kila darasa ni takribani dakika 38.

## II. Maelezo na Kusudi

A. Mafunzo haya ni uchambuzi wa kina katika Waefeso, tukizingatia ukweli wa mafundisho juu ya kanisa na mambo ya kuyatendea kazi katika maisha ya Mkristo.

B. Wanafunzi watapata ufahamu mkubwa wa kitabu hiki, na jinsi kinavyofundisha kuhusu kanisa.

C. Ili kuwa na shukrani nyingi zaidi kwa kuongezwa katika kanisa la Bwana na kutia hamasa kuishi maisha ya kulitukuza jina tunalolivaa kama Wakristo.

## III. Vifaa Vinavyohitajika Darasani

A. Unapaswa kuwa na:

1. Biblia (UV, ASV, KJV, au NKJV),
2. Masomo yote ya video,
3. Notisi za kozi.

B. Maoni:

1. Toleo la tisa la mhadhara “Spiritual Sword” katika kitabu cha Waefeso.
2. Fafanuzi (commentary) yoyote yenye kuzingatia mafundisho ya awali katika Waefeso.

## IV. Kazi Unayopaswa Kuifanya Darasani

A. Soma kitabu kizima cha Waefeso angalau mara tatu.

B. Tazama masomo yote kwa njia ya video.

C. Soma notisi za darasani kwa ujumla wake.

D. Kamilisha kazi yote ya kudondoa (maelezo chini).

E. Wasilisha makala yako ya muhula (maelezo chini).

F. Fanya mitihani miwili.

G. Kiwango chako cha kufaulu kiwe angalau asilimia 70.

## V. Kazi ya Kudondoa

A. Dondoa lazima zidondolewe (au kuchapwa) bila kutazamia mahali popote pale. Uzidondoe kutoka UV kama ulivyoamriwa na sheria za shule.

B. Mistari lazima idondolewe katika mkao mmoja. Unaweza kujifunza zaidi na kuanza upya mistari yote ikiwa umekosea, lakini ni sharti uanze yote upya na kuiandika katika mkao mmoja.

C. Kwa kozi hii, mistari hii inapaswa kudondolewa:
   Waefeso 1:3; 2:8-10; 4:4-6; 5:11; 6:13-18.

D. Dondoa zitatakiwa wakati unatuma mtihani wako wa mwisho.

E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuziandika katika kadi/karatasi ili iwe rahisi kuzirudia mara kwa mara kipindi chote unapochukua kozi hii.

VI. **Mitihani**

A. Kuna mitihani miwili katika Waefeso. Wa kwanza utachukua sura ya 1-3. Na wa pili utachukua sura ya 4-6.

B. Unapokaribia sura ya 3, wasiliana nasi ili utumiwe mtihani wa kwanza. Utakapokaribia sura ya 6, wasiliana nasi ili ufanye mtihani wa pili.

C. Utakapopata mtihani, unaruhusiwa kuuangalia na kujifunza.

D. Lakini, unapoufanya mtihani, unapaswa kuufanya bila ya kuangalia notisi, Biblia na fafanuzi, n.k.

**VII. Makala ya Muhula**

A. Andika mtazamo kwa ujumla wa kitabu cha Waefeso, ukielezea mambo muhimu katika kila sura na kuonyesha masomo tunayoweza kujifunza.

B. Makala yanapaswa kuwa na kurasa sita ikiwa yamechapwa, kwa kuruka mstari mmoja mmoja. Ikiwa utaandika kwa mkono, makala inapaswa kuwa kurasa nane, bila kuruka mstari.

C. Makala uwakilishe juma la mwisho la muhula.

## Mazingira ya Kitabu cha Waefeso

**I. Paulo alipita hapo kwa muda mfupi. Mdo.18:19-21**

A. Aliwaacha Prisila na Akila hapo.

B. Paulo aliingia katika sinagogi na kujadiliana na Wayahudi.
   1. Walimtaka Paulo akae zaidi hapo, lakini hakufanya hivyo akaondoka kwenda Yerusalem.
   2. Paulo aliahidi kurejea hapo tena, "Mungu akijalia."

**II. Apolo anakutana na Prisila na Akila Mdo.18:24-28**

A. Apolo.
   1. Mzaliwa wa Alexandria.
   2. Mtu wa elimu.
   3. Mtu hodari katika maandiko.
      a. Alikuwa amefundishwa njia ya Bwana.
      b. Roho yake ilikuwa ikimwaka.
      c. Alinena na kufundisha kwa usahihi habari za Yesu.
         1) Naye alijua ubatizo wa Yohana mbatizaji.
            a) Ni dhahiri mafundisho yake yalizingatia Agano la Kale bila kujua jinsi ya kutumia vyema yalivyotimia siku zake.

B. Prisila na Akila wakamwelekeza njia ya Bwana kwa usahihi zaidi.

C. Apolo aliyapokea na akaendelea kutumika.

**III. Paulo anarejea Efeso Mdo.19:1-41**

A. Watu kumi na mbili waliokuwa wanafunzi.
   1. Walibatizwa ubatizo wa Yohana – lakini hawakujua habari za Roho Mtakatifu.
   2. Walimsikiliza Paulo na kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo (cf. 1 Sam.25:9 – "*Basi walipofika vijana wake Daudi, wakamwambia Nabali sawasawa na maneno hayo yote kwa jina la Daudi, kisha wakanyamaza"*).
   3. Paulo akawawekea mikono – wakapokea Roho Mtakatifu.
      a. Walinena kwa lugha na kutabiri.

B. Paulo anarejea tena katika sinagogi.
   1. Alinena kwa ujasiri kwa kipindi cha miezi 3.
      a. Akihojiana na kushawishi juu ya ufalme wa Mungu.
   2. Wengine wakakaidi na kukataa kuamini.
      a. Wakaitukana Njia ile mbele za makutano.
   3. Paulo akaondoka na kuwaacha.
      a. Paulo akawatenga wanafunzi.
      b. Akahojiana na watu katika shule ya mtu mmoja, Tirano.
         1) Alifundisha kwa muda wa miaka miwili.
            a) "*Hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani*" (Mdo.19:10). Jambo hili linaweza kusaidia jinsi kanisa la Kolosai lilivyoanza.
         2) Paulo anatenda miujiza.

C. Wana saba wa Skewa (Wayahudi wazururaji).

D. Kuchomwa kwa vitabu (vyenye thamani ya 50,000 za fedha).

E. Mfua fedha, Demetrio, aliyekuwa akitengeneza madhabahu katika hekalu la Artemi.
   1. Akasababisha ghasia kubwa.

F. Baada ya ghasia hizo, Paulo anaondoka kuelekea Makedonia.

**IV. "*Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa*." Mdo.20:17-38**

A. Mwenendo wa Paulo akiwa Efeso.

B. Mahubiri ya Paulo Efeso.
   1. Hakuzuia chochote kilichowafaa.
   2. Hakujiepusha na kuwahubiri habari ya kusudi lote la Mungu.

C. Maonyo ya Paulo:
   1. Jitunzeni,
   2. Mbwa mwitu wakali wataingia kwenu,
   3. Tena watainuka katikati yao, na kulipotosha kundi, na
   4. Kwa hiyo kesheni na kuikumbuka miaka 3 niliyokaa kwenu.

**V. Waraka wa Yesu kwa Efeso Ufu.2:1-7**

A. Sifa (commendation).
   1. Walikuwa na saburi na kufanya kazi kwa ajili ya Kristo.
   2. Hawakuchukuliana na watu wabaya (evil).
   3. Waliwajaribu wale waliojiita mitume – na kugundua kuwa waongo.
   4. Waliyachukia matendo ya Wanikolai.

B. Aliwashutumu (condemned).
   1. Waliuacha upendo wao wa kwanza.

C. Aliwataka watubu.

**WAEFESO – KIPINDI CHA KUANDIKWA WARAKA**

I. Kuinua ari ya kushukuru mpango wa Mungu wa ukombozi.

II. Kuwakumbusha baraka kuu zipatikanazo ndani ya Kristo Yesu.

III. Kutilia mkazo kusudi la Injili.
   A. Huondoa tofauti – Myahudi, Mataifa, n.k.

IV. Kuwahamasisha waishi kwa manufaa ya Injili ya Kristo.
   A. Filp.1:27.

**WAEFESO – SISITIZO KUU**

I. KANISA LA KRISTO
   A. Mtaala wa Kanisa la Agano Jipya.

**YALIYOMO KATIKA WAEFESO**

Kitabu hiki kinaweza kugawanywa katika sehemu kuu mbili zenye sura tatu kila moja.

| | |
|---|---|
| Kwanza | MAFUNDISHO |
| Pili | UTENDAJI AU KUHIMIZA |
| | |
| Kwanza | UKWELI WA MKRISTO |
| Pili | MAISHA YA MKRISTO |
| | |
| Kwanza | NEEMA YA MUNGU |
| Pili | MAONYO KWAO WALIOPATA NEEMA |

NUKUU MBALIMBALI
“Katika kuamua juu ya wengi waliotoa maoni murua, waraka huu ni bora zaidi kupita nyaraka zote za Paulo. Kuna mambo ya kipekee yenye ubora katika mafundisho yake ambayo hugusa akili na kupewa jina la “Waraka wa Kupaa.”

“Sehemu kubwa ni kwa hao wanaongojea mbingu.”

Kenneth S. Wuest, Eph. And Col. in the Gr, N.T.m
Eardman’s Pub. Co., Grand Rapids, Michigan
Dibaji

“Kama matokeo ya kufungwa kwake, hakuna waraka mwingine ulioweza kukamilishwa na mtume isipokuwa huu ambao ni kazi iliyo bora zaidi, wenye kulifaa kanisa wakati wote. Katika waraka huu pekee, zimo sababu zote za kumsifu Mungu, ni nani basi anayeweza kuleta mema katika mabaya na nuru katika giza.”

Charles R. Eerdman
Baker Book House
Grand Rapids, Michigan
INTRODUCTION p. 12

“Kama waraka huu ulikusudiwa kwa Waefeso tu na wao peke yao, ama kwa makanisa mengine yaliyokuwa Asia, au kuzunguka katika jimbo zima, maana ya msingi ni hii: kwamba waraka una ujumbe wenye mambo muhimu na yenye faida ajabu, yaliyolenga kwa mahitaji na hali ya kila Mkristo kwa muda wote na katika kila nchi.”

Charles Eardman
Ibid.
INTRODUCTION p. 16

## WAEFESO – UCHAMBUZI
## SURA YA KWANZA

Paulo anajitambulisha na kutoa salaam ………………………………….. 1:1,2

**Mstari 1.**
“*Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko Efeso wanaomwamini Kristo Yesu*.”

A. “*Paulo*.”
   1. Lugha ya kilatini – dwarfish, dogo, haba.
      a. Matendo 13:9.

B. “*Mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu*.”
   1. David Lipscomb – Rum.1:1-5 “awali ilivyotajwa kazi yake aliyoagizwa.”
   2. Gal.1:1 GHAFULA (abrupt).
      a. Tuchukulie kuwa wewe ni mwalimu wa uongo na unataka kutoamini ujumbe, kuliko kushambulia ukweli uliovuviwa, njia bora ingekuwa kumshambulia mnenaji.
      b. Gal.1:11-24.
   3. Paulo alikuwa mtume – sawa katika mamlaka na uweza na wale kumi na wawili.
      a. Mdo.9:15,16. Chombo kiteule kwangu – alichukue jina langu mbele ya Mataifa, wafalme na wana wa Israeli.
      b. Mdo.22:21 Enenda zako: kwa kuwa mimi nitakutuma uende mbali kwa watu wa Mataifa.
      c. 1 Kor.15:8-10; 2 Kor.12:11,12.

   4. “Zaidi ya nusu ya Agano Jipya limekuwa na kazi, upendo, juhudi na kujitoa wakfu kwa Paulo kama mtume wa Kristo” (Johnny Ramsey).

   5. TOFAUTI.
      a. Flp.1:1; Tito 1:1; Film.1.
         1) Maelezo haya yanaonyesha sawa na mtumwa maskini kabisa ambaye alimtii Mungu.

        2) Watu wote husimama wakiwa sawa chini ya msalaba.
            a) Math.11:11.
    b. Hili ni fumbo.
        1) Rum.6:16-18.

C. "*Kwa watakatifu walioko Efeso*."
1. Wakristo wote wanaweza kuitwa "watakatifu."
    a. Kuitwa hivi zaidi ya kuwa "Wakristo" au jina lingine lolote.
    b. Waliotakaswa, watakatifu, walikuwa wakfu, waliotengwa kando.

2. Neo la Kiyunani – "HAGIOS." Inaonekana kuwa moja ya maneno ambayo Ukristo wa Agano Jipya huinua na kutendea kazi kwa namna ya kipekee.

3. 1 Pet.2:9; Tito 2:14; Yoh.15:19.
    a. Yak.4:4; 1 Yoh.2:15-17.

4. 1 Kor.1:2.
    a. SIO TU SUALA LA UZOEFU KIKAZI – BALI NI KWELI.

D. "*Wanaomwamini* (faithful) *Kristo Yesu*."
1. Hili si kundi tofauti na lile la watakatifu, bali wasifu wengine.
    a. Mtazamo aina mbili kuhusu "uaminifu."
        1) Kutumaini au kustahili kutegemewa.
        2) Kusadiki, au kuwa na imani, katika Kristo.
            a) Yakobo 2:14-16.
            b) Ufunuo 2:10; 1 Kor.4:2.
            c) Yohana 1:12.
2. Tutalijadili hili zaidi tutakapofika mstari wa 3.

**Mstari wa 2**.

A. "*Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo*."
1. Paulo alitumia salaam ya kawaida kwa namna ya kuadhimisha.
    a. Sifa kwa kuheshimu desturi za siku hizo zimegeuzwa na mitume katika baraka zote za Mkristo.
        1) Neema – huruma bila kustahili.
            a) Palipo na neema, kisha amani hufuata.
2. Asili ya neema na amani.
    a. "Hakika kuna mkazo madhubuti juu ya maoni sahihi katika kujua asili ya baraka hizi. Baba ndiye 'Mungu wa neema zote' (1 Pet.5:10) na 'Mungu wa amani' (Ebr.13:20); na ni sawa kwamba 'neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo' (Yoh.1:17), 'naye ndiye amani yetu' (Efe.2:14). Lakini Baba ndiye kiini cha chemichemi ya baraka zote kwa wanaoamini" (D. Lipscomb).

**Baraka za Rohoni Katika Kristo**

Kuanzia mistari ya 3-14 tutaona maneno muhimu na yenye changamoto katika misamiati ya Ukristo.

| | |
|---|---|
| Kufanywa wana (adoption) | Urithi |
| Ukombozi | Kutiwa muhuri (sealed) |
| Kuchaguliwa kabla (foreordained) | Wokovu |

Kwa maana pana ni kwamba baraka hizi hupewa Wakristo kulingana na kusudi la milele , - na wala si ovyo ovyo tu. Ni matokeo ya nia na mpango wa Mungu. Ukweli huu huzidisha uzito wa baraka, "Awezaye kutenda mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo" tukisema kama Paulo katika Waefeso 3:20.

**Mstari wa 3**.

A. "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo*."
   1. "*Atukuzwe*" (blessed).
      a. "EULOGETOS" – Kutoka neno la Kiyunani ambalo tunapata neno "eulogy"; lenye maana "kumnenea mema, kusifia."
         1) 2 Kor.1:3; 1 Pet.1:3.
         2) "EULOGETOS" limetumika tu likimlenga Mungu katika Agano Jipya.
      b. MAANA – "Hebu na Mungu, Baba wa Bwana Yesu Kristo anenewe mema; asifiwe."
      c. "Kwa kusifia utukufu wa neema ya Mungu."
   2. "*Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo*."
      a. Hubainisha ubinadamu wa Kristo.
         1) Math.27:46 "Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti…Mungu wangu, Mungu wangu…"
      b. Kumbuka kila nafsi katika Uungu inamtambua kila mmoja kuwa sawa na kuita Mungu kila mmoja kwa mwingine.
         1) Ebr.1:8; Zab.45:6,7.
      c. Yesu ni Mwana kwa namna ya kipekee (unique sense).
         1) Yoh.5:17,18.
      d. "Hakuna mwanadamu ambaye ataelewa jambo hili kikamilifu – LAKINI KRISTO ALIKUWA WAKATI MMOJA NI MWANADAMU NA MUNGU."

B. "*Aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni*."
   1. Yakobo 1:17.
      a. A-L-L – HAKUNA MAHALI PENGINE TUNAWEZA KUPATA HIVI.
   2. Rum.8; Flp.4.

C. "*Katika ulimwengu wa roho*."
   1. Haswa "Katika ulimwengu wa mbinguni."
      a. "Hili linarejea kanisa la Kristo na uhusiano uliotukuka ambao Mungu ameuleta katika Kristo" (D. Lipscomb p.17).
   2. Msemo huu unapatikana mara 5.
      a. Efe.1:3,20; 2:6; 3:10; 6:12.
         1) Halipatikani mahali pengine popote katika Biblia.
   3. Msisitizo ni nini?
      a. Waebr.9:24; Mdo.7:56; Ufu.3:21.
      b. Angalia mistari maalum 1:20 na 2:6.
      c. "Kristo ameinuliwa katika ulimwengu wa mbinguni, na hao wote walio 'ndani yake' ni wa ulimwengu wa mbinguni pia (F.F. Bruce, p. 27).
         a) Flp.3:20; 1:27; Efe.2:19; 1 Pet.2:11.
   4. Inaonekana kama Paulo anasema baraka zote za rohoni asilia zenye faida milele zinapatikana tu "ndani ya Kristo," ambaye yuko mbinguni, ambako wewe uko kwa maana ninyi ndio hufanya mwili wa Kristo.
      a. "Baraka" hizi za "rohoni" ni kwa ajili ya hao wanaofaa mbinguni: zinatusaidia kuandaa mbingu, na asili yake ni mbinguni.

D. "*Katika Kristo*."

1. Kumbuka mazingira yote.
2. Rum.8:1; 2 Tim.2:10; 1Yon.5:11; Ufu.14:13.
    a. Ni jinsi gani tunaingia ndani ya Kristo?
        1) Ubatizo wa kiroho!

**Mstari w 4**.

A. "*Kama alivyotuchagua katika yeye*."
1. Hebu na tutambue mambo ambayo tunayaona hapa.
    a. Mtu au baadhi ya watu wamechaguliwa.
    b. Waefeso ni kundi au miongoni mwa makundi hayo.
    c. Wamechaguliwa "katika yeye."
2. Jambo la pili na tutambue mambo tusiyoyaona.
    a. Hatuoni iwapo uchaguzi una masharti ama la.
    b. Hatuoni iwapo ni mtu mmoja mmoja au kundi zima.

B. "*Kabla ya kuwekwa misingi ya uimwengu*."
1. Mdo.15:18; Efe.3:9.
    a. Kila kimoja kimekusudiwa na Mungu wetu.
    b. Jambo hili si suala mbadala (after-thought).

C. "*Ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia*."
1. 1 Pet.1:16.
    a. Kumbuka Efe.1:1.
    b. 1 Thes.5:23; Flp.2:15.
2. Imetendeka namna gani hiyo?
    a. 1 Pet.1:22.
    b. Yak.4:4; 2 Kor.6:14ff; 1 Pet.4:4; Efe.5:11.
3. Ni eneo gani la maisha hugusa na hili?

**Mstari wa 5.**

A. "*Kwa kuwa alitangulia kutuchagua*."

**KUTANGULIA KUTUCHAGUA** (Predestination)

1. Rejea katika makala – "Studies in 1 and 2 Thessalonike and Philemon" Katika Kujibu Mafundisho ya Uongo (1)" na Don Walker

2. Pia angalia makala – "Kitabu cha Waefeso" Salaam na Dua; Kutoa Sifa Kutokana na Baraka za Mungu kwetu, kwa Njia ya Injili, katika Kristo – Sawasawa na Kusudi lake la Milele (1:1-14)" na Hugo McCord.

3. Maneno mawili ya Kiyunani:
    a. "PROORIDZO."
        1) Limetumika mara mbili katika Efe.1:1-14.
        2) Limetamfsiriwa "kutangulia kuchaguliwa" au "kukusudia kabla."
        3) Likimaanisha kutia alama kabla, kuamua kabla.
        4) Marejeo ya Maandiko:
            a) 1 Kor.2:7 "*Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu*."
            b) Mdo.428 "Hekima hiyo ilihitaji kifo cha Kristo ambacho ni "mashauri ya Mungu yaliyokusudiwa tangu zamani yatokee."

c) Rum.8:29,30 Mungu "aliwachagua tangu asili" Wakristo (kuitwa, kuhesabiwa haki, kutukuzwa) ili wafananishwe na Yesu, ndugu yao mkubwa.
d) Efe.1:5 Mungu "alitangulia kuchagua" kwamba wenye dhambi (watoto wa Ibilisi, Yoh.8:44) wangefanywa (adopted) kuwa wana wa Mungu.
e) Efe.1:11 Urithi wao hao waliofanywa kuwa wana si suala lililokuja ghafula. Bali, "*sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri lake la mapenzi yake*."
5) Ukiangalia katika rejea hizo hapo juu hakuna hata moja inayoonyesha kwamba kutangulia kuchaguliwa huzingatia uamuzi wa mwanadam na wajibu wake.

b. "EKLEGO."
1) Efe. 1:4.
2) Limetumika kuonyesha hao ambao Mungu amewachagua (wateule wake).
3) Ikimaanisha kuweka kando, kuwatenga, kuchagua.
4) Rejea za Maandiko:
a) Lk.14:7; 10:42; Mdo.13:17; Rum.11:7; Math.22:14; Ufu.22:17; Rum.8:23,24.

4. Yoh.10:16; Mdo.18:9,10.
a. Math.16:24,25; Mk.8:34,35; Lk.9:23,24.
b. Math.11:28-30; Ufu.3:20.
c. Kumbuka mfano wa mpanzi (Lk.8).
1) Ni jinsi gani imetimilika?
a) Angalia Efe.1:13.
(1) Yoh.1:12; 8:32; Mdo.20:32.

5. IKIWA FUNDISHO LA KALVINI NI KWELI:
a. Hukumu yao wasioteuliwa ni sawa tu na kutangulia kujua tamko la upendo wake kwao walioteuliwa na kupata wokovu.
1) 2 Tim.2:4; 2 Pet.3:9.
b. Yesu hakujua basi hilo!
1) Math.11:28; Mk.16:15,16; Ufu.3:20.
c. Kwa nini basi tufanye kazi hizi?
1) Kuhubiri injili? Rum.1:16.
2) Tuhimize watu watubu? 2 Pet.3:9; Mdo.17:30; Lk.13:3.
3) Tufundishe kwamba neno la Mungu huokoa? Yak.1:21.
4) Hata tuhitaji neno la Mungu? 2 Tim.3:16,17.
5) Ikiwa kuna jambo hata dogo linalonipasa nifanye, kwa nini nilazimike kufanya hilo? Mdo.9:6; Ebr.5:8,9.
6) Wangewezaje watu kuwa na nguvu hata za kufanyika wana wa Mungu kama hawawezi jambo lolote? Yoh.1:12.

6. "Muhtasari: Mungu alitangulia kujua na kuchagua kabla mpango wa wokovu; alipanga kabla, masharti, mambo, malengo na makusudi ya mpango mzima wa ukombozi. Lakini, kila mtu amewekwa huru afanye uamuzi binafsi, kwamba atakubali ama kuukataa mpango wa Mungu. Mungu anataka kila roho iokolewe. Lakini uamuzi wa mwisho ni kwa kila mtu; Mungu atamwajibisha kila mtu kwa uamuzi atakaoamua" (T. Cummings).

7. Mungu amewachagua aina ya watu ambao mioyo yao inarutuba katika Neno la Mungu (Lk.8). Watalipokea Neno hilo, wataliamini Neno, watatii Neno na hivyo basi kuchaguliwa kwa kufanywa wana "adoption" (Efe.1:5).

B. “*Ili tufanywe wana*.”
1. Yoh.1:12; Gal.4:1-7; Rum.8:16, 17; Efe. 5:1.
2. Kufanyika wana ni hatua ya kisheria ya kumfanya mgeni awe na haki kama watoto wa kuzaa.
    a. Hebu tuone matumizi yake:
        1) Tulikuwa hatuna cha kudai kwa Mungu.
            a) Efe.2:1-3.
                1) Ni mwenendo gani tuliuendea?
                    (a) Tulizaliwa bila hatia – tukatengwa – tukakombolewa.
                2) Tendo ni lile la upendo safi na ulio mkuu.
                    a) Efeso 2;4-6.
                3) Sasa tuko chini ya ulinzi na uangalizi wake.
                4) Lazima tuwe na roho ya kuwa wana, tuonyeshe utii.

C. “*Kwa njia ya Yesu Kristo mwenyewe*.”
1. Kufanywa wana huku kumewezekana kwa sababu ya kazi ya ukombozi ya Kristo.
    a. Gal.4:4-6.
2. Kwa kusudi la Mungu.

D. “*Sawasawa na uradhi wa mapenzi yake*.”
1. Haikuwa katika uwezo wa mwanadamu, wala si katika mashauri yake. Haikutegemea kustahili kwake mwanadamu au matendo yake mema.
    a. Rum.11:33-36.

**Mstari wa 6**

A. “*Na usifiwe utukufu wa neema yake*.”
1. Ni namna ya Kiebrania.
    a. Kwa jina lake lililotukuka.
        1) Lengo ilikuwa ni kuchochea shukrani kwa neema yake Mungu iliyotukuka ambayo imedhihirika katika wokovu wake mwanadamu.

2. Ukweli kwamba Mungu ameanzisha njia na mpango ambao mwanadamu anaweza kuonja baraka ambazo kwa kawaida zitachochea shukrani.
    a. Hata hivyo, mara nyingi hakuna kinachochochea zaidi isipokuwa kubeza.

B. “*Ambayo ametuneemesha.*”
1. Efe.2:11-13.

C. “*Katika huyo Mpendwa*.”
    1. Math.17:5.

**Mstari wa 7.**

A. “*Katika yeye huyo, kwa damu yake*.”

**UKOMBOZI**

1. Mambo matatu juu ya ukombozi.
    a. Kitu ambacho ulikimiliki kwanza kikapotea.
    b. Fidia imetolewa ili kurea tena.
    c. Nguvu zimevunjwa.

2. Hebu tuchunguza haya sasa:

a. Kitu ambacho awali ulikimiliki kimepotea.
    1) Math.18:3; Isa.59:1,2.
b. Fidia imetolewa ili kurejeza tena.
    1) 1 Pet.1:18,19; Efe.1:14; 1 Kor.6:19,20.
c. Nguvu imevunjwa.
    1) Mk.3:27; 1 Kor.15:55-57.

3. Kwa damu yake.
    a. Ebr.9:22; 10:4.
    b. Isa.1:18; Zek.13:1.
        1) Math. 26:28; Kol.1:14; Ufu.1:5; Rum.5:9; 3:24:25.

B. "*Masamaha ya dhambi*."
1. Ebr.1:13; Isa.59:1,2.
    a. 2 Kor.5:21; Mk.15:34.
2. Yer.3:25; Rum.6:23.
    a. Rom.3:10; 1 Yoh.1:8,10.

C. "*Sawasawa na wingi wa neema yake*."
1. Wingi (riches) ikimaanisha kupita kiasi (superfluity) – zilizojaa tele.
    a. Ambazo zinazidi kiwango cha mwanadamu anachohitaji na kutaka.
        1) Angalia matumizi yake katika mafungu mengine
            a) Efe.1:18; 2:7; 3:8; 3:16.
            b) Rum.2:4; 9:23; 11:12; 11:33.

2. Neema.
    a. 2 Kor.8:9.
        1) Neema ya Mungu haiwezi kupungua.

**Mstari wa 8.**

A. "*Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote*."
1. Anazungumzia kuhusu neema.
    a. Haijafungwa, bali ni huru (liberal) na imejaa tele.

B. "*Katika hekima yote." "*
1. Mungu ameidhihirisha hekima yake kubwa katika mpango wa wokovu.
    a. Alibuni mpango ambao ni mahiri mno kwa kumwokoa mwanadamu.
    b. Hekima ni kumwokoa mwanadamu ili adumishe heshima ya Sheria yake mwenyewe.
        1) Hekima ya Mungu isiyo na kikomo imeonekana kwa namna ambayo haridhii:
            a) Kati yake mwenyewe na mwanadamu.

2. 1 Kor.1:20,21.
    a. Yakobo 3:13-18.
        1) Kuangalia kulingana na jinsi Mungu anavyoona.

C. "*Na ujuzi*" (prudence). Neno sahihi hapa lingekuwa "busara."
1. Mithali 1:1-6 (ASV).
    a. Wakati hekima ni suala la ndani lililo la kawaida, busara ni uwezo wa kutambua mambo ya kutenda katika kuona matokeo yake.
        1) Hekima ni nadharia, busara ni utendaji (practical).

   b. Basi maana yake ni kwamba Mungu alifahamu na kuelewa hekima halisi hivyo akaitekeleza ili kupata matokeo aliyokusudia.
      1. Busara ni kuitendea kazi hekima.

**Mstari 9**.

A. "*Akisha kutujulisha siri ya mapenzi yake*."
   1. "Siri" – MUSTERION.
      a. Jambo fulani ambalo mtu ni lazima alianzishe kabla ya kujulikana wazi.
         1) Kutoka katika neno MUEO – kuanzisha au arifu (instruct).

      b. KUTOWEZA KUKABILI SIRI
         1) Ni jambo lililo nje na utaratibu wa asili wa kuelewa.
         2) Inaweza kujulikana tu kwa njia ya ufunuo. Imejulikana kwa njia na wakati ambao Mungu alipanga.

   2. Maneno yanaambatana na "siri."
      a. "Kutujulisha", "kudhihirishwa", "kufunuliwa", "kuhubiriwa", "kuelewa", "mpango wa Mungu."

   3. Kol.1:26; Efe.6:19,20.

   4. Siri ni jambo pana lenye kujumuisha mambo mengi.
      a. Kol.1:27 (Kristo).
      b. Efe.3:4-6 (Wayahudi na Mataifa kuwa mtu mmoja).
      c. Efe.1:9,10 (mpango wa Mungu).

   5. Mpango wa Mungu ikiwa pamoja na kuwajumuisha Mataifa katika kanisa, Kristo akiwa ndiye kitovu (center) cha mpango mzima wa Mungu.
      a. Hii ni siri ya injili – WALA SI KANISA TU.
         1) 1 Tim.3:16; Efe.3:9,10.
   6. Kanisa halikuwa siri – bali lilijumuishwa katika siri kama sura ambayo ingekuwa ndiyo majumuisho ya mambo yote mbinguni na duniani.

B. "*Sawa sawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo*."
   1. Ilijulikana na Mungu kwa muhula wake.
      a. 2 Tim.1:9,10.
   2. Kudhihirika kwa siri hiyo ilihabarisha hekima izidiyo hekima yote nyakati za nyuma.
      a. Efe.3:4,5; 1 Kor.2:6-9; Kol.2:2,3.

**Mstari wa 10**.

A. "*Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu*."
   1. "Wakati" – OIKONOMIA.
      a. Kimsingi inaashiria uongozi wa nyumba.
         1) OIKOS – nyumba, NOMOS – sheria.
         2) Uwakili.
      b. Lakini hapa au katika 3:9 "fellowship" (KJV) lina maana tofauti kidogo.
         1) Mpangilio, muundo uliowekwa au maongozi ya Mungu.
            a) Mpangilio au utaratibu ulioundwa kwa mpangilio, au hata mwisho huu. Uliundwa kwa ukamilifu huu akilini.
               (1) USISAHAU mstari wa 8.

2. "Wakati mkamilifu."
    a. Ukamilifu wa wakati mara nyingi inahusisha kuja Yesu mara ya pili.
        1) Hata hivyo , inaweza kuna maana zaidi ya hiyo.
            a) Gal.4:2,4; Ebr.1:12; 9:10; 1 Pet.1:20; Rum.5:6.
            b) Yoh.2:4; 7:6; 12:20-23; 17:1.

        2) Pointi ni kwamba Mungu alipanga matukio kwa wakati na historia ili akamilishe mpango wake. Mungu anaratibu.

B. "*Atavijumuisha vitu vyote katika Kristo*."
1. ASV – (To sum up all things in Christ).
    a. Ni nini hatima ya mpango huu wa Mungu?
        1) YESU KRISTO.
            a) Kol.1:16-20.
                (1) Kol.3:11; Ufu.5:13.

C. "*Vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia*."
1. Ukuu wa utawala wa Kristo.
    a. Math.28:18.
        1) Kuvipatanisha viumbe vyote vikaavyo mbinguni na duniani.
            a) Haswa, kwa watakatifu duniani.
                (1) Viumbe vya mbinguni havipaswi kubadilika. Bali wanadamu lazima wahesabiwe haki na kuendana na hali ya mbinguni.
                    (a) Flp.2:9,10.

D. "*Katika yeye huyo*."

**Mstari wa 11**.
A. "*Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi*."
1. ASV – (We were made an heritage).
    a. Kuna dhana mbili muhimu kuhusu "sisi."
        1) "Hao ambao kwanza wameongolewa, bila kujali rejea ya kwamba awali walikuwa Wayahudi;- mitume na watenda kazi pamoja nao." (Barnes Notes pg. 973.)

        2) Ni Wayahudi. Mstari wa 13 ni Mataifa.
            a) Rum.1:16.
            b) "Israeli ilitazamwa kama urithi na fungu la Bwana. Kanisa kwa kuwa limeundwa na Israeli mpya sasa linapata fursa ile ile."
                (1) Rum.8:17; Gal.3:29; Kol.1:12.
                (2) Kumb.32:29 "*Maana, sehemu ya Bwana ni watu wake, Yakobo ni kura ya urithi wake*."

B. "*Huku tukichaguliwa tangu awali tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye*."
1. Angalia notisi katika mistari ya 4 na 5.
    a. Kuna sheria za kiroho zinazofanya kazi sawasawa na sheria zozote za mwili.

C. "*Kwa shauri la mapenzi yake*."
1. Jambo lolote Mungu analoamua lazime litimie.
    a. KUMBUKA mstari wa 8.

**Mstari wa 12**.

A. "*Tupate kuwa sifa ya utukufu wake*."

1. Kusudi kubwa la mwanadamu ni kumtukuza Mungu.
   a. Mhu.12:13; Efe.3:21; Isa.43:7.

B. "*Sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu*."

1. Kuna mambo mawili tunayotakiwa kuyaangalia.
   a. Umuhimu wa neno la Mungu kwa ajili ya wokovu.
      1) Rum.10:17; Yoh.20:30,31; 1 Pet.1:23.
      2) Yoh.6:63,68; Yak.1:21,22; Mdo.20:32.

   b. Angalia jinsi "neno", "ukweli" na "injili" yalivyounganishwa pamoja na kutajwa kama mamoja na yenye kuendana.
      1) Injili ni uweza wa Mungu uwezao kuokoa (Rum.1:16), bali neno lilipandwa ndani yenu linaweza kuokoa roho zenu (Yak.1:21).
      2) Katika 2 Yoh.9 tunasoma, "*Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundishio hayo, huyo ana Baba na Mwana pia*."
         a) Kuna jambo ambalo ni lazima tulifanye na kwa ufupi ni "neno la kweli, habari njema za wokovu wenu."

C. "*Tena mmekwisha kumwamini yeye*."

1. Marudio ya "katika yeye" hutufanya kumwangalia Kristo (Efe.1:3).
2. Biblia wakati wote huunganisha imani na utii pamoja mithili ya imani ilivyo.
   a. Angalia mtu mmoja mmoja katika Waebrania 11.
   b. Yak.2:14-26.

D. "*Na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu*."

1. Mdo.2:38; 5:32; 1 Kor.6:19,20; Efe.1:13.
   a. Jinsi gani?
      1) Mdo.2:38; 5:32 kwa kulitii Neno.
      2) Kol.3:16.
   b. Mdo.6:1-8.
   c. Je, kuwa na Roho ni kufanya ishara?
      1) Lk.1:15; Yoh.10:41.

**Mstari wa 14.**

A. "*Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu*."

1. Angalia pia 2 Kor.1:22,23.
   a. Ikiwa rehani au dhamana haijalipwa kwa kuendeleza basi imepotea pamoja na bidhaa iliyolipiwa.

2. Arabuni (earnest) ni neno lililotumika kwa pete ya posa. Uchumba huvunjika kila mara.

3. Nyaraka hizi ziliandikwa kwa Wakorintho na Waefeso (Wakristo).
   a. 1 Kor.9:27.
      1) "Kukataliwa" ikimaanisha kunyang'anywa ushuhuda wako wa sasa na kuzuiwa kupokea zawadi yote (W.E. Vine).
   b. 1 Kor.10:12; 2 Kor.12:21 na Lk.13:3.

c. 2 Kor.13:5; Yer.6:20.

4. Ufunuo 2:1-5.
   a. Mdo.20:28-32.
   b. Iliandikwa toka Efeso 1 Tim.1:19,20.
   c. 1 Tim.4:1-3.
   d. 1 Tim.6:10.
   e. 2 Tim.4:10; 1 Yoh.2:15-17.

5. Kama Ibilisi angeweza kuushawishi ulimwengu wote wa dini kwamba hatuwezi kuanguka, angeweza kutubembeleza sote tulale.

6. Mafungu mengine yanayojadili mada hii:
   a. Yoh.10:27-29.
      1) Changanua maneno: vitenzi vimekuwa katika wakati uliopo; kadiri kondoo zinavyofuata hazitapotea (Ufu.14:4).
      2) Hakuna kitu kinachoweza kututenganisha na Mungu isipokuwa kutokuwa waaminifu.
   b. 1 Petro 1:5.
      1) Neno hili ni sawa na lililotumika katika 2 Kor.11:32 likimaanisha mji uliolindwa. Lakini Paulo aliokoka kwa kupitia ukutani.
      2) 1 Pet.5:8,9; 2 Pet.2:20-22; 1:4-11; 3:17.

7. Mafungu haya yanathibitisha kuwa tunaweza kuanguka kutoka katika neema.
   a. Math.13:48-50; Mdo.8:19-24; 927; 1 Kor.9:27; 10:12; 2 Kor.12:21; 13:5; Gal.5:4; 1 Tim.1:19;20; 4:1-3; 6:10; 2 Tim.4:10; Ebr.4:1,2; 10:38, 39; Yak.5:19,20; Yoh.8:21; 1; 2 Yoh.8; Yuda 21; Ufu.2:1-5; 3:1-5.

B. "*Ili kuleta ukombozi wa milki yake*."
   1. Angalia notisi katika mstari wa 7.
   2. Mdo.20:28; Efe.5:25; Math.16:18.

C. "Kuwa sifa ya utukufu wake."
   1. Kusudi zima la mwanadamu ni lipi?
   2. Kumtukuza Mungu.

**Mstari wa 15.**

A. "Kwa sababu hiyo mimi nami."
   1. Katika mambo niliyosema tayari, angalia mistari ya 13 na 14.

B. "*Tangu nilipopata habari za imani yenu katika Bwana Yesu*."
   1. Efe.1:1
   2. Imani hapa si ile ya awali imwongozaye mtu wokovuni bali ni utendaji wa siku kwa siku katika Bwana katika maisha ya kila siku.
      a. Rum.1:17; Ebr.11:6.
      b. Gal.5:6; 1 Thes.1:3.

C. "*Na pendo lenu kwa watakatifu wote*."
   1. Gal.5:22.
   2. 1 Pet.2:17; Yoh.15:12,13; 1 Kor.16:14.
   3. 1 Thes.1:3.

        a. Ni jinsi gani imani na upendo huu ulijulikana?
            1) 1 Yoh.3:18.

D. Jambo lingine la nyongeza.
    1. Wengine hudai:
        a. Katika Kol.1:4 tunaona jambo linalolingana. Kwa kuwa Paulo hakuwahi kuwaona ndugu katika Kolosai, tunapaswa kuhitimisha kuwa hata hawa ndugu hakuwahi kuonana nao. Tunatambua alikaa Efeso kwa miaka mitatu (angalia Matendo). Hivyo basi, waraka huu haukuandikwa kwa ajili ya Waefeso.
        b. Tatizo la dhana hii:
            1) Katika Filemoni 5, tunaona maneno kama haya na wazo linalolingana kabisa. Filemoni aliongolewa na Paulo mwenyewe.
            2) Pengine hakukutana nao tangu alipokutana na wazee Mileto (Mdo.20:17).

**Mstari wa 16.**

A. "*Siachi kutoa shukrani kwa ajili yenu*."
    1. Paulo alijua namna ya kufurahia uaminifu wa wengine.
        a. 2 Yoh.4; 3 Yoh.3.
        b. Hili linaweza kuamsha matendo mema fulani upande wetu.
            1) Sisi, kama Wakristo, lazima tuwajibike katika maisha ya watu wengine.
                a) 1 Yoh.3:18.

B. "*Nikiwakumbuka katika sala zangu*."
    1. Flp.4:6; 1 Thes.5:17.
    2. 1 Tim.2:1.

**Mstari wa 17.**

A. "*Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu*."
    1. Wakati wote Paulo alimwomba Baba, hakuwahi kumwomba Yesu.
        a. Efe.3:14; 5:20.
            1) Mkristo ni lazima awe anatambua katika kutofautisha kazi za Mungu baina ya nafsi za Uungu.
        b. Ni kazi ya Baba tu, yeye pekee, tunayepaswa kusali mbele zake.

    2. Tunapaswa pia kutambua Mk.15:34 na Yoh.20:17.
        a. Yoh.1:18.
        b. Kol.2:9.

    3. Efe.1:22,23.
        a. "Kwetu sisi, Mungu ni Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo kama alivyokuwa nyakati za kale kwa Israeli, Mungu wa Abraham, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo" (Lipscomb).

    4. Mungu anastahili sifa na utukufu.
        a. Rum.6:4.
            1) Math.5:16.
            2) Angalia mistari 19,20.

B. "*Awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye*."
    1. Ni aina gani ya sala hii? Maombezi (intercession).
        a. Kusihi kwamba Mungu angewapatia "roho."

1) Je, hii ni rejea juu ya "Roho Mtakatifu" au "Roho ya mwanadamu" au mwenendo wa kiroho au majaliwa (endownment)?
   a) Tafsiri ya KJV – "the."
   b) ASV – "a."
      (1) Kutokuwepo kwa "article" ni jambo zuri ikionyesha anayelengwa si Roho Mtakatifu.
         (a) Angalia pia kwamba katika KJV "article" imeandikwa kwa herufi ndogo.
         (b) Katika Wakolosai 1:9, tuna maelezo yanayolingana.
            (a) Ili kuwa na "roho" hiyo, mtu inampasa awe na roho yenye tabia ya hekima na ufunuo utokao kwa Mungu.

   c) Baadhi ya mambo yanayopinga kuwa "roho ya mwanadamu" kwa sababu anayeitoa ni Mungu.
      1) Paulo anaomba roho zao zipate kuwa na sifa au tabia fulani zilizo bora.
         (a) Rum.11:8 – Mungu huleta roho ya usingizi. Kwa nini asiweze kuleta kinyume chake – "roho ya hekima?"
            [1] Yakobo 1:5; 1 Fal.3:9.
         (b) Roho ya Mkristo inatajwa kuwa:
            [1] 1 Kor.4:21; Gal.6:1; 2 Tim.1:7.
               [a] Tabia za roho ya mwanadamu kama zilivyoshawishiwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye ndiye.

   d) Mtu huipata tabia hiyo kama Paulo alivyoomba kama baraka zitokanazo kutokana na utii kwa Kristo – angalia 1 Kor.1:23,24.

C. "*Katika kumjua yeye*."
   1. "Kumjua" – EPIGNOSIS – ni zaidi ya neno la kawaida la elimu.

   2. "*Macho yenu yatiwe nuru*."
      a. Kuelewa – SUNESIS – Kol.1:19.
         1. 2 Tim.2:7.

      b. 1 Yoh.5:20, kuelewa kwamba Yesu hutoa:
         1) Ebr.8:10; 10:16.
         2) Yoh.8:32 hoja ya moja kwa moja mstari wa 31.

      c. Kutiwa nuru huku hakufanyiki kimiujiza kutoka kwa Roho Mtakatifu.

      d. Yohana 1:9.
         a) 2 Tim.1:10.
            (1) Efe.3:8-10.
               (a) 2 Kor.4:4 – Ibilisi.
               (b) 2 Kor.4:6 – Mungu
               (c) 2 Kor.10:5 – Mwanadamu
                  [1] Efe.5:8,11; 1 Yoh.1:7.

      e. Mbali na sala, Mungu atahifadhi mioyo na nia" (Flp.4:7). Ni sala tu ambayo Paulo anaitoa hapa kwa Wakristo Waefeso.

C. "*Mpate kujua*."

1. Hapa Paulo anataja kusudi alilokuwa nalo.
    a. Anatamka “nini” (whats) tatu.
        1) Ni nini tumaini la wito wenu?
        2) Ni nini utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu.
        3) Na ni nini ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tunaoliamini?
2. Wito, urithi, na uweza.
    a. Haswa akimaanisha:
        1) “Tumaini” la wito wake.
        2) “Utukufu” wa urithi wake.
        3) “Ukuu” wa uweza wake.

D. “*Wito wa tumaini lake*.”
1. Upendo umetajwa nusu mara nyingi kama imani.
2. Tumaini limetajwa kwa sehemu mara nyingi kama upendo.
    a. Tumaini ni neno la ufunguo katika Agano Jipya na ni muhimu kwa Mkristo kuwa na matumaini.
        1) Efe.2:12 kuwa Mataifa.
            a) Efe.4:4.

    b. Nia na madhumuni.
        1) 1 Pet.1:13 tumaini moyoni mwake.
            a) Kol.1:5 tumaini lililowekwa mbinguni.

        2) Tito 2:13; Ebr.6:18.
            a) Rum.8:24.
            b) 1 Tim.1:1 haswa “tumaini letu.”

E. “*Na utajiri wa utukufu wa urithi wake*.”
1. 1 Kor.3:21,22.
    a. Kwa sababu Rum.8:17.

2. Urithi wa Mkristo kimsingi ni baadaye. Mk.10:30.
    a. Ebr.9:15.
    b. Mwisho wa dunia, Wakristo: Kol.3:24; 1 Pet.1:4.

3. Paulo si tu anataka wasomaji wake watambue hilo, bali pia kuelewa “ utajiri wa utukufu” wake.

**Mstari wa 19**.
“*Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake*.”

A. “*Na ubora wa ukuu wa uweza wake*.”
1. Uweza – DUNAMIS
    a. Dynamic, dynamite.

2. Alipenda wajue uweza wake si tu katika:
    a. Miujiza (Gal.3:5), na
    b. Karama maalum kwa mitume (Efe.3:7), lakini
    c. Pia hupatikana kwa Wakristo wote, Efe.1:19.
        1) Efe.3:16.

        2) Ni uweza mkubwa ndani ya nafsi, ambao huleta tabia kuwa na "saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha" (Kol.1:11).

   3. Ukuu wa uweza "uzidio" – kuingia katika maeneo mengine.
      a. Ni nguvu nyingi hizi.

B. "*Ndani yetu tuaminio*."
   1. Yoh.1:12; Yoh.3:16.

C. "*Kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake*."
   1. Si tu Paulo anataka wasomaji waone uweza huu, bali pia anawataka kuelewa "ni nyingi mno" (exceeding greatness).
   2. Ili abainishe wazi wingi wa nguvu zake, Paulo anatumia pamoja maneno manne yanayofanana.
      a. "Nguvu" (Power) – DUNAMIS – kwa kadiri ya "utendaji" – ENERGEIA- wa nguvu (mighty) KRATOS) za uweza (power) – ISCHUS).
         1) Hivyo basi tunaweza kuona uweza mkuu wa Mungu ukielezwa.

**Mstari wa 20**.
"*Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho*."

A. "*Aliotenda katika Kristo*."
   1. Uweza wa Mungu umedhihirika katika matukio mawili:
      a. Kwa kumfufua Kristo kutoka kwa wafu, na
      b. Kumketisha Kristo mkono wa kuume wa Mungu.

B. "*Alipomfufua katika wafu*."
   1. Kifo cha Kristo kilidhihirisha upendo mkuu wa Mungu (Rum.5:8; Yoh.3:16), kadhalika ufufuo ulidhihirisha uweza wake Mungu.
   2. "Ni nguvu nyingi za Mungu au 'utendaji' (DUNAMIS) aliotenda (EBERGEO) katika Kristo zinaweza kutenda kazi 'ndani yetu' kiroho "kuliko yote tuombayo au tuwazayo" (Efe.3:20).
      a. Wafilipi 3:10.

C. "*Akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho*."
   1. Ufufuo na kuketishwa kitini Kristo ni mambo mawili aliyoinuliwa kwayo (Mdo.2:32).
      a. Mdo.7:39.

   2. Zab.110:1.
      a. Mdo.2:34; Ebr.1:13.

   3. Maelezo ya "ulimwengu wa roho" angalia 1:3.

**Mstari wa 21.**
"*Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwengu humu tu, bali katika ule ujao pia*."

A. Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani."
   1. Falme za kawaida.
   2. Wengine wanadhani kuwa anarejea cheo juu ya malaika.

   a. Lakini katika Kol.1:16, maneno matatu kati ya manne (isipokuwa nguvu) yametumika juu ya viumbe "vinavyoonekana" na "visivyooneka" vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya "nchi."
   b. Math. 28:10 wala si "malaika" tu, bali pia wote wenye "mamlaka na nguvu" wamewekwa chini yake (1 Pet.3:22).

B. "*Na kila jina litajwalo*."
   1. Wafilipi 2:9.

C. "*Wala si ulimwenguni humu tu, bali na katika ule ujao pia*."
   1. Hakika "anastahili Mwana-kondoo" (Ufu.5).

Mistari ya 22,23.
"*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote*."

A. Yafuatayo yanatoka katika kitabu cha "Spiritual Sword Lectureship" katika "Kitabu cha Waefeso." Alitoa mhadhara huu ni Gary Workman wenye kichwa "Sala ya Paulo" (1:55-23), pp.21-25.

**Uongozi wa Kristo**.

"'*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake*.' Maelezo haya yanarejea wazo la nyumba. Akishaonyesha uweza wa Mungu katika ufufuo na kuketishwa kwa Kristo kitini pa enzi kumesababisha kwa kawaida kabisa kuwa Bwana wa dunia nzima (mst.22a) na pia kiroho (22b). Kwa kuwa Kristo ni "juu sana" kuliko yeyote, haiwezekani kupinga kwamba vitu vyote viko chini ya miguu yake.' Lakini Paulo haachi hata kitu kimoja. Anapenda wasomaji wake wajue kwamba Mungu alionyesha uwezo huo kwa kumfufua na kumketisha Yesu kitini pa enzi kisha 'kuvitiisha' vitu vyote chini yake. Maneno toka (22a) yanalingana na Zaburi 8:6, ambao kwa asili unarejea kwa Adam. Lakini Maandiko yanahusisha utimilifu kamili wa mtu wa kwanza ukitimia katika Adamu wa pili – Yesu (1 Kor.15:27; Ebr.2:8). Hata hivyo, hautatimia kikamilifu hata atakaposhindwa adui wa mwisho – mauti (1 Kor.15:26), maana "sasa hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake' (Ebr.2:8). Mwishoni, kutiishwa vitu vyote chini ya Yesu isipokuwa tu Mungu Baba (1 Kor.15:27), ikirejea hapa kwamba ni Mungu aliyemketisha na kuviweka vitu vyote chini yake.

*"'Akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa*.' Fungu hili (22b) linahusisha mtajo wa kwanza kabisa wa 'kanisa' katika Waefeso. Neno hilo katika Kiyunani EKKLESIA, ambalo ndilo limetoa neno 'kanisa' hupatikana mara 115 katika Agano Jipya. Wakati mwingine linarejea mkusanyiko wa kidunia na mara nyingine katika mkutano wa Wakristo wa ibada. Kawaida, hata hivyo, limetafsiriwa kuwa 'kanisa' mara nyingi kwa maana ya kusanyiko moja au mengi ya mahali maalum. Lakini mara tisa zinazopatikana katika Waefeso (1:22; 3:10,21; 5:23,24,25,27,29,32), zinamaanisha kanisa kwa maana ya dunia nzima. Ni dhahiri, 'mwili mmoja' imetajwa maalum (Efe.2:16; 4:4). Matumizi ya neno EKKLESIA lina asili yake katika maelezo ya Yesu: 'Nitalijenga kanisa langu' (Math.16:18).

"Maelezo ya mwisho ya mstari wa 22 ni baadhi ya mafungu yetu yanayoleta shida katika kutafsiri. Angalia KJV (gave them to be head,' ambako maneno (to be) yameandikwa kwa herufi za mlazo (italicized). Kwa kuwa maneno hayo hayapo katika maandishi ya Kiyunani, wengine wanadhania badala yake yangekuwa 'as.' Katika kutafakari, 'kichwa juu ya vitu vyote' ni mbadala wa maneno 'vitu vyote kuwa chini ya miguu yake' kutoka sehemu ya kwanza ya mstari iliyotangulia. Paulo alikuwa akisema, 'Mungu alimweka Yesu (kuwa kichwa juu ya vitu vyote) katika kanisa.' Kwa sababu hiyo, Yesu kuwa kichwa juu ya kanisa haijaelezwa moja kwa moja, ila kwa kuhusisha

kwamba Mungu ‘akamweka ’ Yesu katika kanisa kama mwenye mamlaka yote juu ya wote. Wanaotafsiri hivi huelekeza maelezo ya Paulo katika Wakolosai 2:10 ambapo Kristo ametajwa kuwa ‘kichwa cha enzi yote na mamlaka’ (maneno mawili yote yaliyotajwa katika Efe.1:21). (Tafsiri imeungwa mkono na Arndt-Gingrich Lexicon, Blaikie Puilpit Commentary, Hendriksen, Lenski, et al.)

“Kuna sababu za kupinga tafsiri hiyo hapo juu. Isipokuwa katika Wakolosai 2:10 (na pengine 1 Kor.11:13), rejea nyingine zote ni Kristo kama ‘kichwa’ zimeungaishwa pamoja na kanisa. Ni ‘jiwe kuu la pembeni’ katika nyumba ya Mungu ya kiroho (Math.21:42; Mk.12:10; Lk.20:17; Mdo.4:11; 1 Pet.2:7). Yeye ni ‘kichwa’ kilichoundwa pamoja na ‘mwili’ (Efe.4:15,16; Kol.2:19). Na ametambulishwa haswa kuwa ni ‘kichwa cha mwili, kanisa’ (Efe.5:23). Hivyo basi tungeelewa neno “akamweka” kwa maana ya ‘kuteuliwa,’ – kwamba Mungu ‘alimteua kuwa kichwa cha juu cha kanisa’ (NEB). Kati ya tafsiri 13 zilizoangaliwa, 7 zinatafsiri ‘akamweka’ (gave) –EDOKEN- kuwa ama ‘kuteuliwa,’ ‘kufanywa,’ au ‘kuwekwa,’ yenye maana kwamba Mungu ‘alimweka katika kanisa kuwa kichwa juu’ (TCNT). Kwa hali yoyote ile, karibu tafsiri zote zinaelewa ‘kichwa’ katika fungu hili kuwa ni kichwa cha kanisa.

“Baadhi ya watoa fafanuzi (commentators) wanataka kuwa na njia zote mbili, wengine hupendelea hivi: ‘Limepewa kanisa, na kwa ajili ya faida ya Kanisa, Kichwa ambaye pia ni juu ya vitu vyote’ (Farancis Foulkes, The Epistle of Paul to Ephesians, Eerdmans, 1963, p.65). Hata hivyo, pasingeonekana kuwa na kupatana kuelewa ‘kichwa’ kwa maana mbili. Jambo la ziada ni kwamba Paulo ameshakwisha kusema tayari kuwa Yesu ni mwenye mamlaka yote juu ya viumbe vyote. Maelezo haya katika mstari wa 22 hutia nguvu ukweli kwamba ndiye Bwana wa kiroho juu ya kanisa – alifanywa ‘kichwa cha mwili,’ kanisa ili kwamba awe mtangulizi katika yote (Kol.1:18). Ukweli ni kwamba, yeye ni ‘Bwana mmoja’ aliyenenwa katika Waefeso 4:4-6 ambako ‘mwili mmoja’ umetajwa.

‘“*Ambao ni mwili wake*.” Katika baadhi ya barua za awali za Paulo, watu miliki za Bwana wametajwa kama mwili (Rum.12:4,5; 1 Kor.10:17; 12:12-27). Ingawa inaeleweka kwamba ‘mwili’ umetajwa kuwa kanisa (linga. 1 Kor.12:27 pamoja na mst. wa 28), kutambulisha ‘kanisa’ kama ‘mwili’ limebainishwa wazi hapa (Efe.1:22,23), tena katika mpangilio wa nyuma mbele (reverse), katika Wakolosai 1:18, 24. Kanisa halijaiitwa tu ‘mwili wake’ bali ‘mwili wa Kristo’ (Efe.4:12; linga. 1 Kor.12:27), maana ni kutoka katika Kristo aliye kichwa mwili huo unaweza kukua (Efe.4:15,16). Ni katika nyaraka pacha za Waefeso na Wakolosai ambapo sitiari (metaphors) za Yesu kuwa ‘kichwa’ na kanisa kama ‘mwili wake’ yameunganishwa pamoja. Na kwa kuwa ‘kichwa’ na ‘mwili’ Paulo katika maelezo yake ameunganisha pamoja, ni dhahiri kwamba Kristo kuwa kichwa hailengi tu nafasi ya yake kama Bwana, bali pia hunena muungano muhimu sana ambao upo kati yake na watu wake.

‘“*Ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote*.” Sehemu hii ya mwisho ya sala ya Paulo pengine ndiyo muhimu zaidi kuliko fungu zima na hakika hali ya utata kujaribu kuelewa. Imetajwa kuwa ‘eneo gumu,’ ‘fungu lenye kuzua maswali mengi,’ maelezo ambayo tafsiri zake ‘zimeleta ushindani’ na mjadala ‘unaojadiliwa kwa kurasa nyingi za watoa fafanuzi.’ Sehemu kubwa ya kwanza ya tafsiri ni maelezo yafuatayo: (1) Kristo amefanywa mkamilifu na Mungu, (2) Kristo amefanywa mkamilifu na kanisa, (3) kanisa limekamilishwa ama na Kristo au Mungu. Mjadala umezingatia sehemu kubwa katika maana ya ‘ukamilifu’ (PLEROMA), ama kitenzi cha kuendelea PLEROUMENOU mwishoni mwa mstari ukinamaanisha ‘kukamilisha’ (filling) au ‘kukamilishwa” (being filled).

Tafsiri ya kwanza kwa ustadi imepingwa na Merick. (F. Meyrick, ‘Ephesians,’ The Bible Commentary, F.C. Cook, ed. Eerdmans, ilichopwa tena 19981.) Kuanzia mwanzo kabisa kutoka

Yohana 1 ambapo Yesu ametajwa kuwa ‘amejaa’ neema na kweli (mst.14) na hivyo basi akiwa na ‘ukamilifu’ wa Uungu (mst.16). Ni kweli pia kwamba ndani ya Kristo ‘hukaa utimilifu wote Mungu’ (Kol.2:9; linga. 1:9). Kwa kuwa Paulo ananena ‘utimilifu wote wa Mungu’ (Efe.3:19) na ‘utimilifu wa Kristo’ (Efe.4:13), neno linasema kiteolojia likionyesha ukamilifu katika Mungu. Kwa mtazamo huu, maneno ‘ambalo ndilo mwili wake’ yametengwa (parenthesis), na ‘ukamilifu’ hurejea kwake (Kristo). Fungu linalolingana na hilo ni Kol.1:17,18) limetolewa kuchangia, ambapo Paulo, baada ya kusema Yesu ni ‘kichwa cha mwili, kanisa,’ anarejea nyuma kwa Yesu kwa maneno yanayofuata. Lakini, Paulo anaingiza kiwakilishi ‘ambaye’ (who) katika Wakolosai ili kubainisha dhahiri. Maelezo katika Waefeso yangeongeza mpangilio mbaya wa muundo wa sarufi, bila kutia chumvi, ikiwa tafsiri hii ni sahihi.

“Tafsiri ya pili kwa ustadi imepingwa na Robison na siku za karibuni, Abbott. (J. Armitage Robinson, Commentary on Ephesians, Kregel, iliyorudiwa kuchapwa 1979; T.K. Abbott, ‘Epistles to the Ephesians and Colossians,’ The International Critical Commentary, T & T. Clark, 1897. Angalia pia Barry [Ellicott’s Commentary], Lenski, Hendriksen, Bruce, et al.). Mtazamo huu unazingatia kwamba ‘ukamilifu’ lazima ichukuliwe kwa maana ya kauli tendi (active sense) ya kitu kinachokamilisha kuliko kuweka katika maana ya kauli ya kutendwa (passive sense) ya kile kilichokamilishwa. Kwa kubainisha zaidi, imenenwa kwamba ‘ukamilifu’ katika fungu letu inaonyesha ‘kile kinachokamilisha’ hivyo basi kanisa ni ‘ukamilifu’ wa Kristo. Tafsiri nyingine zimeshirikisha mtazamo huu katika tafsiri zao za fungu hili (Weymouth, Knox, NEB). Moja ya msingi wa tafsiri hii ni maoni kwamba mwisho wa mstari kuna kauli yenye kitenzi endelezi (passive participle) na hivyo humzungumzia Kristo ‘ambaye vyote katika vyote vimekamilika’ na kanisa na vitu vyote, au ‘ambaye daima amekamilishwa’ na Mungu. Mtazamo ambao ulitazamwa na baadhi ya tafsiri za kale na watoa maoni. Lakini mtazamo huu si sahihi, umejengwa juu ya sarufi isiyosahihi kuielewa. Wala mtazamo huo kwa ujumla wake hauonekani kulingana na mazingira ya fungu (kadhalika na Agano Jipya zima) kuwakilisha Kristo analifanyia nini kanisa, na wala si kanisa linamfanyia nini Kristo.

‘“Tafsiri ya tatu ni mtazamo sahihi. Inaungwa mkono na Arndt-Gingrich na Thayer Lexicon, na kwa ustadi inatetewa na Salmond na Foulkes. (Salmond, Foulkes, kama tulivyoona tayari. Angalia Robertson, Blaikie, et al., na haswa Lightfoot katika fafanuzi zake za Wakolosai.) Dhana hii inachukua ‘ukamilifu’ katika kauli ya kutendwa (ambayo imekamilishwa) katika kuvumisha (modifying) kilichorejewa na kiwakilishi cha karibu (immediate antecedent) – ‘mwili,’ kama kawaida kabisa. Katika Waefeso, Paulo analiwakilisha kanisa kuwa linakua hata kufikia ‘ukamilifu wa Kristo’ (Efe.13-16) na hakika ‘kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu’ (3:19). Paulo alisema pia kwamba ‘katika yeye (Kristo) mmetimilika’ (Kol.2:10), na Yohana alisema kwamba ‘kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea’ (Yoh.1:16). Na kwa kuwa lilikuwa kusudi la Mungu ‘kuvijumuisha vitu vyote pamoja katika Kristo’ (Efe.3:19), na kwa kuwa Mungu amesema, ‘Je! Mbingu na nchi hazikujawa nami?’ (Yer.23:24), pengine ni Mungu Baba ambaye Paulo anasema, ‘anayekamilika kwa vyote katika vyote.’ Kwa maana hiyo, kanisa limewakilishwa na Paulo kuwa ukamilifu wa Mungu. Kwa vyovyote vile, dhana hii ingelikuwa ya ki-Maandiko na kweli. Basi, katika kuhitimisha bayana juu ya utukufu wa kanisa kwa sababu ya mambo linalopata kutoka kwa Mungu mwenyewe, mtume anahitimisha sala hii. Tunaweza kuitikia tu ‘Ameni.’

## WAEFESO SURA YA PILI

Tunapoingia sura ya pili ni lazima tuelewe kwamba Paulo hajaacha mada alioijadili, bali sasa anafafanua pointi katika mstari wa 19, - UKUU WA UWEZA WA MUNGU. Mungu alidhihirisha uweza wake kwa kumfufua Yesu kutoka kwa wafu. Angalia tofauti alizotambulisha – Kristo alikufa – lakini akafanywa kuwa hai. “*Nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu*” (Ufu.1:18).

Paulo, katika sura hii atatumia tofauti hiyo hiyo kadiri tunavyotafakari maana ya kiroho. Nanyi mmehuishwa (haswa, mmefanywa hai), ninyi mliokuwa mmekufa katika makosa na dhambi zenu – (Efe.2:1). Paulo ataonyesha ni jinsi gani Mungu alivyowatwaa watu ambao kiroho walikuwa wamekufa wasiofaa kitu na kuzitumia nguvu zake kwa namna ambayo huwaweka pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho, na kuwajenga pamoja kuwa maskani ya Mungu.

**Mstari wa 1.**
"*Nanyi* [mmehuishwa] *mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu*."

A. "Nanyi [mmehuishwa]" – KJV.
   1. Kol.2:12,13; 3:1.

   2. Maneno haya haswa yanamaanisha "amewafanya kuwa hai."
      a. Yoh.5:21; Rum.4:17.
      b. Yoh.10:10; 14:6.

      3. "Nguvu zile zile ambazo ziliwekwa juu ya mwili mfu wa Kristo na kumfufua kutoka kwa wafu hata kumketisha kitini mkono wa kuume wa Mungu zimewekwa juu yao hao waliokufa katika makosa na dhambi zao ili washiriki pamoja kwa njia ya imani utukufu wa uzima wa milele" (D. Lipscomb, p. 38).

B. "*Mlikuwa wafu kwa makosa na dhambi zenu*."
   1. 1 Thes.5:6; Ufu.3:1; Math.8:22; Lk.15:24,32.
   2. Rum.6:23; Isa.59:1,2.

Mstari wa 2.
"*Ambazo mlizitenda zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi*."

A. "*Ambazo mlizitenda zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu*."
   1. Yoh.15:19; Rum.12:1-2.
   2. 1 Yoh.2:15-17; Yak.4:4; 1 Pet.4:4; 2 Kor.6:14-7:1.
   3. Yoh.18:36.

B. "*Kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga*."
   1. Zaidi sana hili linarejea kwa shetani.

   2. Katika mafungu mbalimbali anarejea katika lugha mithili ya hii.
      a. "Mkuu wa mapepo."
         1) Math.9:34; 12:24; Mk.3:22; Lk.16:11.

      b. "Mkuu wa ulimwengu huu."
         1) Yoh.12:31; 14:30; 16:11.

   3. Mbali ya kuwa watumishi wa haki, walikuwa watumishi wa dhambi (Rum.6:17,18).

C. "Roho yule atendaye kazi katika wana wa kuasi."
   1. Ibilisi anafanya kazi ndani ya maisha ya hao wana wa ulimwengu.
      a. 1 Pet.5:8,9.

**Mstari wa 3**.
"*Ambazo zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine*."

A. "*Ambazo zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu*."
   1. "…tulikuwa wote katika hali moja, katika hali ya taabu, si mara moja tu kujitosa katika dhambi, bali tukatumia muda wote kwa kuishi katika tamaa za mwili, zisizokoma, bali katika kutimiza matamanio ya mwili, kama kulikuwa hakuna jambo lingine kabisa zaidi ya kutimizia matakwa ya mwili wa asili (Lipscomb, p. 40).

   2. 1 Yoh.2:15-17; Gal.5:19,20.

B. "*Tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na nia*."
   1. Ni maisha mabaya mwanadamu kuyatenda ambaye aliumbwa kwa sura ya Mungu (Mwa.1:26, 27).
      a. Gal.5:19-21.

   2. Katika kutumia Maandiko dhambi za 'mwili,' 'ulimwengu,' na 'ibilisi' sio madaraja tofauti ya dhambi, bali ni aina mbalimbali za dhambi, na kila moja kati ya maadui watatu wakubwa hao imefanyika ikiwakilisha zote" (Lipscomb, pp. 40,41).

C. "*Tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine*."
   1. Imebainishwa kiurahisi kabisa, hali isiyobadilishwa.
      a. Hii ndiyo hali ya kwanza kuwa "wafu katika dhambi" (2:1,5).

   2. Hili si suala la kuzaliwa katika dhambi. (Angalia notisi za Kuzaliwa Dhambini.)
      a. Tunachotakiwa kutambua ni kwamba Paulo anaonyesha tofauti dhahiri. Ni tofauti kati ya kuwa wafu dhambini na kuwa hai kwa Mungu. Katika mazingira haya tunaona dhahiri kabisa. Angalia jedwali hapa chini.

**UTOFAUTISHAJI WA PAULO**

| **WAFU KATIKA DHAMBI** | **KUFANYWA HAI** |
|---|---|
| Tulienenda – katika tabia za ulimwengu | Mungu ni mwingi wa rehema |
| Tulienenda – mkuu wa uwezo wa anga | Mungu ana upendo mwingi |
| Watoto wa kuasi | Tulihuishwa pamoja na Kristo |
| Tamaa za mwili | Tumeokolewa kwa neema |
| Tukitimiza matakwa ya mwili | Tumefufuliwa |
| Tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira | Kuketi na Kristo ktk ulimwengu wa roho |
| Kama na hao wengine | Tumeonyeshwa wingi wa utajiri wa neema yake |

**Mstari 4.**
"*Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda*."

A. "*Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema*."
   1. Kwa sababu ya dhambi tulikuwa kukielekea katika maangamizi.
      a. Rum.6:23; Isa.591,2; Yer.3:25.

   2. Ingawa, "lakini" imetia mkazo.

a. Katika saa ya mwanadamu ya giza Mungu akamletea tumaini.
   1) Mwa.3:1-15.
   2) Mangamizi ya mwanadamu yalififia kadiri nuru ya rehema ya Mungu ilivyokuwa ikiangaza.
      a) "Utajiri" ikilenga kufurika au kujaa tele.
      b) Hakuna kitu cha kupungukiwa.

B. "*Kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda*."
1. "Lakini Mungu."
   a. Njia walizozifuata wanadamu ni za hatari. Mwisho wake ambao ni kifo hakiepukiki (Rum.6:23). Jawabu, kwa hiyo, lazima liwe jawabu lenye nguvu nyingi.
   b. Neno "lakini" ni kutilia mkazo. Inarejea nyuma njia ambayo mistari ya 1-3 imeidhinisha.
      1) Mungu, Mungu pekee ndiye jawabu!

2. "*Kwa kuwa ni mwingi wa rehema*."
   a. Rehema – Mungu anashindwa kumpatia mwanadamu anachostahili.
      1) 2 Pet.3:9; Rum.12:1,2.
      2) Mungu wa rehema.
         a) Hosea 2:19.
         b) 2 Kor.1:3.
         c) Mik.7:18.
         d) Zab.51:1; Rum.9:23.

3. "Kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda."
   a. Upendo ndiyo sababu kuu.
      1) 1 Yoh.4:8.
         a) Yer.31:3.
         b) Rum.8:38,39 (upendo usioonekana).

   b. Upendo wa Mungu dhidi ya ule wa mwanadamu
      1) Upendo wa mwanadamu una upendeleo. Tunawapenda rafiki zetu, na kuwachukia maadui zetu.
      2) Mungu anawapenda maadui zake na kuwafikiria kuwatendea mema.
         a.) Rum.5:6-8.
      3) Rehema na upendo wa Mungu huangaza zaidi hata wakati tunaangalia mstari wa kwanza hadi wa tatu.

**Mstari wa 5.**

A. "*Hata wakati tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu*."
1. Angalia maelezo 2:1.

B. "*Alituhuisha pamoja na Kristo; yaani tumeokolewa kwa neema*."
1. Agano Jipya huunganisha uhusiano baina ya Kristo na mwuumini.
   a. Tumesulubiwa pamoja naye. …………………………….. Gal.2:20.
   b. Tunakufa pamoja naye. ………………………………….. Rum.6:5
   c. Tunafufuka pamoja naye. ………………………………… Kol.3:1-3.
   d. Tunaishi pamoja naye. …………………………………….. Flp.1:21.
   e. Tunatawala pamoja naye. ………………………………… 2 Tim.2:12.
   f. Ni washirika wa urithi. …………………………………… Rum.8:16,17.
   g. Tunashiriki mateso duniani. ………………………………. Flp.1:29.

h. Tutashiriki utukufu wake katika kiti cha enzi …………….. Ufu.3:21.

C. "(Mmeokolewa kwa neema).
1. Wakati huu tutajaribu kuanzisha mada na kuijadili kwa kina katika mstari wa 8.
a. 2 Kor.8:9.
b. Ryum.6:23.
c. Ebr.2:9.
d. Tito 2:11,12.

2. Neema ni huruma mtu asizostahili – Mungu anapotukirimia tusichostahili.

**Mstari 6.**
A. "*Akatufufua pamoja naye*."
1. Lazima tukumbuke uweza wa Mungu usio kifani (Efe.1:19,20).
a. Nguvu ile ile iliyodhihirika kwa ufufuo wake Kristo na kumketisha kitini pa enzi ndiyo inayodhihirika juu ya Wakristo.

B. "Akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu."
1. Mahali ni mbinguni (heavenly places).
a. Kol.3:1-3.
b. Yoh.14:1-3; Ebr.9:27.
1) Ufu.14:4.
c. Flp.3:20.
d. Math.6:19ff.

2. Katika Kristo Yesu.
a. Efe.1:3.
b. Rum.8:1.
c. 2 Tim.2:10.
d. 1 Yoh.5:11.
e. Ufu.14:13.
f. 1 Kor.12:13; Gal.3:27,28.

**Mstari wa 7.**
A. "*Ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu*."
1. HII NIA KWA KUSUDI LA MUNGU KUU LA KUTUKUZWA.
a. Mhub.12:13; Rum.12:2.

**Mstari wa 8**.
A. "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu*."
1. Rum.3:23; 6:23.
2. 2 Kor.8:9.
a. Flp.2:6-10.
3. Lk.19:10; 1 Tim.1:15.
4. "NEEMA YA MUNGU YA AJABU."
a. Mafungu mbalimbali.
1) Efe.2:8-16. "Kupatanishwa" yaani "kufanywa mmoja."
2) Tito 2:11,12; 3:4-7.

3) Rum.5:6-9.
4) Yoh.3:16; 1 Tim.2:4-6.
5) Yoh.1:17.

b. Neema hufafanuliwa - mapenzi mema, huruma, zawadi, rehema iliyotolewa (yote hiyo asiyostahili mwanadamu). Neema ni pale Mungu anapotukirimu mambo tusiyostahili. Rehema ni pale ambapo hatutendei jinsi tunavyostahili.

c. Aina tatu za kutoelewa:
   1) MTAZAMO WA MAFARISAYO JUU YA SHERIA.
      a) Mafarisayo, katika akili zao, hawakumwitaji mwokozi. Walidhania kuwa wangejiokoa wenyewe kwa njia ya sheria.
         (1) Mk.2:17ff.
         (2) Rum.9:33.
         (3) Gal.5:11.

   2) KANISA LA KATOLIKI LINADAI WOKOVU KWA NJIA YA MATENDO MEMA
      a) Lk.17:10 watumishi wasiostahili.
      b) 1 Kor.15:10 kwa njia ya neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo.

   3) WENGI WANATUSHUTUMU (KANISA LA KRISTO) KWA MAONI YAYO HAYO. Lakini tunaamini kile ambacho Paulo alisema na kutenda.
      a) Mdo.9:6ff; 22:16 pamoja na Efe.2; Tito 3.
         1) Kol.2:12 imani katika utaratibu wa Mungu.

      b) Efe.2:8; Rum.1:6; Mdo.20:24.
         1) 2 Thes.1:7-9 kisasi kwao wasiomjua Mungu na wao wasiotii injili.

      c) Kwa unyenyekevu tunaikubali neema ya Mungu kwa kutenda yanaambatana na neema.

d. Neema inafafanuliwa: Neema ni kitu pasipo kustahili; mwanadamu hastahili, na hawezi kuipata yeye binafsi. Asili yake sio mwanadamu, bali ni Mungu. Ni jambo ambalo mwanadamu hawezi kuipata kutokana na jitihada yake binafsi (Rum.11:33-36).
   1) Nuhu na safina.
      a) Mwa.6; Ebr.11:7; 1 Pet.3:20; 2 Pet.2:5.
         (1) Nuhu angeweza kuwa na imani.
         (2) Nuhu angeweza kujenga safina kwa imani.
         (3) Nuhu angeweza kuhubiri ukweli.
         (4) Nuhu angeweza kuishi kwa haki.
         (5) LAKINI MUNGU ALITOA NAFASI KWA SABABU YA NEEMA YA MUNGU.
         (6) "NUHU, AKIWA NA IMANI, ALIFANYA ALICHOAMRIWA NA MUNGU." – BIBLE TREASURES, pp. 306-310 na Johnny Ramsey.

      b) Efe.2:9; 5:11.
      c) Kol.1:21.
      d) 2 Tim.1:9.
      e) Tito 1:16.
      f) Ebr.6:1; 9:14.

   2) Imetumika katika maana huru (neutral sense).

a) 2 Kor.11:15 "*Mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao*."
b) 2 Tim.4:14 "*Iskanda, mfua shaba, alionyesha ubaya mwingi kwangu; Bwana atamlipa sawasawa na matendo yake*."
c) Ufu.20:12,13 "*Wakahukumiwa …sawasawa na matendo yao*."
d) 1 Kor.3:12-15.

3) MWISHO: Neno "matendo" limetumika katika njia mbalimbali katika mazingira tofauti, kuzingatia mazingira.

B. Mfano unaotusaidia kupambanua.
1. Mwa.15:6 wa Abraham unasema, "*Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki*."
a. Paulo ameutumia mstari huu katika Rum.4:3 na Gal.3:6.
b. Yakobo ametumia nukuu hii katika Yakobo 2:23.
1) Ni dhahiri kwamba Paulo na Yakobo hawalengi jambo moja kwa kutaja neno "matendo."

2. Katika Mwanzo26:5 Yehova anazungumza kwa mwana wa Abrahamu, Isaka, na kumweleza kwa nini alimbariki Abrahamu. Angalia jinsi Maandiko yanavyosema. "*Kwa sababu Ibrahim alisikia (obeyed) sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu*."
a. Angalia jinsi imani (belief, Mwa.15:6) na matendo (obeyed) na kuifadhi maagizo, amri, hukumu, na sheria zangu yanavyoendana.

C. Si kwa matendo ya sheria.
1. Paulo analiweka bayana hili anaposema tumeokolewa si kwa matendo ya sheria katika Waefeso tunapojifunza Wagalatia 3.
a. Katika mazingira haya Paulo kimsingi anatofautisha kuhesabiwa haki kwa imani katika Kristo kinyume na kuhesabiwa haki kwa Sheria ya Kale. Kama Paulo anavyoeleza katika Wagalatia 2:21, "*Siibatilishi neema ya Mungu; maana , ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure*."

D. HITIMISHO:
1. Je, mwanadamu huokolewa kwa matendo mema? Ndiyo. Kwa kuihuisha imani yake kwa njia ya kutii Neno la Mungu.
2. Je, mwanadamu huokolewa kwa matendo ya sheria? Hapana. Ingekuwa hivyo, Kristo amekufa bure (Gal.2:20,21).

**Mstari wa 9.**
A. "*Wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajivuna*."
1. SWALI: Biblia inamaanisha nini kwa neno "matendo?" Je, inawezekana kuwa kwamba katika mazingira mengine neno linamaanisha kitu kingine wakati mahali pengine inamaanisha maana tofauti kabisa?"
a. Ni kwamba tu inawezekana, bali hivi ndivyo haswa.

2. katika mstari huu Paulo anasema wokovu wetu si kwa matendo, wakati Yakobo 2:24 tunasoma, "*Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake*."
3. Angalia masomo maalum katika "Imani na Matendo."

**Mstari wa 10**.

A. "*Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema*."
   1. "Maana tu kazi yake" (POIMA) – Neno la Kiingereza "poem." Hubainisha kilichofanywa. Rum.1:20.
      a. Flp.2:12,13.
      b. Rum.9:20,21.
      c. 1 Kor.3:1-9.

   2. "Tuliumbwa" (KTIZO) – Katika maandiko inamaanisha kuumba, daima ikidhihirisha utendaji wa Mungu.
      a. Kiasili – Rum.1:25.
      b. Kiroho – Efe.2:10,15; 4:24; Kol.3:10.
         1) Yoh.3:1-7.
            a) 1 Pet.1:23.
            b) Yako.1:18.
            c) 1 Thes.2:13.
            d) Kol.3:16.
            e) Kumbuka mazingira yote.

   3. Kwa nini tumekombolewa?
      a. Yer.7:1-7.
      b. Yako.1:21,22.

   4. "*Tuliumbwa …tutende matendo mema*."
      a. Yako.2:19.
      b. Mdo.10:38.
         1) Ebr.12:2; 1 Pet.2:20; Flp.2:5.
      c. Ebr.5:8,9.
         1) Yoh.4:34; 5:19,30,36; 6:38.
         2) Lk.2:49.

B. "*Ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo*."
   1. Paulo anaanzisha maelezo muhimu ambayo tutayakuta sura ya 3:9-11 kuhusu kusudi lake la milele.
   2. "Tuenende."

## MAFUNZO MAALUM
## IMANI NA MATENDO

A. UTANGULIZI:
   1. Je, mwanadamu ameokolewa kwa matendo mema?
   2. Je, mwanadamu ameokolewa kwa matendo ya sheria?
   3. Je, maelezo ya Paulo katika Warumi 4:4, "*Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni*."hubatilisha hitaji la kuhuishwa kwa imani yetu na kutii Neno la Mungu?
   4. Je, Yakobo analenga jambo moja kwa kusema "matendo" katika Yakobo 2 kama vile Paulo anavyomaanisha "matendo" katika Warumi 4 na Waefeso 2?

B. MAUDHUI:
   Tutajitahidi kujibu hoja hizo na maswali mengine katika mtazamo wa Kibiblia.

C. MWILI:
1. Kwanza angalia matumizi ya Biblia ya neno kwa maana tofauti.
   a. Matendo muhimu na mema.
      1) Rum.13:3 – Watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema.
      2) Efe.2:10 – Tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema.
      3) 1 Tim.6:18 – Matajiri wawe matajiri katika matendo mema.
      4) 2 Tim.3:17 – Maandiko hutukamilisha tupate kutenda matendo mema.
      5) Ebr.10:24 – Tukahimizane katika upendo na kazi nzuri.
      6) MAFUNGU MENGINE:
         a) 1 Tim.2:10; 5:10; 5:25.
         b) 2 Tim.2:14.
         c) Yako.3:13.
      7) YAKOBO 2.
         a) Mst.wa 14 – "Je! Ile imani yaweza kumwokoa?"
         b) Mst.wa 17 – "Imani isipokuwa na matendo imekufa nafsini mwake."
         c) Mst.wa 18 – "Imani hujulikana kwa njia ya matendo."
         d) Mst. wa 20 – "Imani pasipo matendo imekufa."
         e) Mst.wa 21 – "Abraham alihesabiwa haki kwa matendo alipomtoa Isaka."
         f) Mst.wa 22 – "Kwa matendo imani yake ilikamilishwa."
         g) Mst.wa 24 – "Alihesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, si kwa imani peke yake."
         h) Mst.wa 25 – "Rahabu alihesabiwa kuwa ana haki kwa matendo.
         i) mst.wa26 – "Mwili pasipo roho umekufa, kama vile "imani pasipo matendo imekufa."

   b. Maovu au matendo yasiyofaa (sio lazima kwa asili au kiini – bali katika utendaji).
      1) Rum.3:27 – "Kujisifu kwa matendo ya sheria?"
      2) Rum.4:2 – "Haukuhesabiwa haki kwa matendo ya sheria."
      3) Rum.4:6 – "Haki pasipo matendo."
      4) Rum.9:11 – "Kuchagua si kwa sababu ya matendo."
      5) Rum.11:6 – "Lakini ikiwa ni kwa neema, haiwi kwa matendo tena."
      6) Gal.2:16 – "Mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria."
      7) Gal.3:2 – Msipokee Roho kwa matendo ya sheria."
         a) Mdo.5:32 – Mungu huwapa Roho wote wamtiio. (Angalia pia Matendo 2:38).
      8) Gal.3:5 – "Usifanye hayo kwa matendo ya sheria."
      9) Gal.3:10 – "Walio wa matendo ya sheria wako chini ya laana."
      10) MAFUNGU MENGINE
         a) Rum.9:32; 13:12.
         b) Efe.2:9; 5:11.

   c. Tuenende nayo."
      1) Efe.2:10 – "Tuenende katika matendo mema."
      2) Efe.4:1 – "Mwenende kama inavyoustahili wito wenu."
      3) Efe.4:17 – "Msienende kama Mataifa waenendavyo."
      4) Efe.5:2 – "Mkaenende katika upendo."
      5) Efe.5:8 – "Enendeni kama watoto wa nuru."
      6) Efe.5:15 – "Mwenende kwa uangalifu."

**Mistari ya 11,12 –** Paulo anatoa rejea juu ya dharau ya Wayahudi kwa Mataifa (wasiotahiriwa).
1. "Kabla ya Kristo, halikuwepo tumaini la umoja.
2. Ndani ya Kristo waliunganishwa.

A. Paulo atatoa muhtasari katika mafungu matano ya hali yao isiyo na matumaini.
    1. "Wakati huo walitengwa na Kristo."
        a. Efe.1:3; Rum.8:1; 2 Tim.2:10; 1 Yoh.5:11; Ufu.14:13.

    2. "Walifarakana na jamii ya Israeli."

    3. "Wageni wasio na maagano ya ahadi."
        a. Abrahamu (Mwa.12:2,3; 15:8-21; 17:1-21).
        b. Watu chini ya Musa (Kut.24:1-11).
        c. Agano Jipya lingechukua nafasi ya lile la kale (Yer.31:31-34; Ebr.8:6-13).

    4. "Mlikuwa hamna tumaini."
        a. Rum.8:24.

    5. "Hamna Mungu duniani."
        a. Mliabudu miungu mingi (Mdo.17:16-31).
        b. Pengine walimjua Mungu (Rum.1:18-23).
        c. 1 Kor.8:5,6.

B. Ni jambo la huzuni kwamba wanadamu walijikuta wenyewe katika mazingira ambayo ni nje ya Kristo.

Paulo ameelezea hali mbaya ya Mataifa (nao wote walio nje ya Kristo) katika mistari iliyotangulia. Sasa atajadili mambo yaliyotukia kwao.

**Mstari wa 13 -** "*Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo*."
    1. Angalia tofauti hizi za kustaabisha.
        a. Awali walitengwa na Kristo.
            1) Sasa wako ndani ya Kristo.
        b. Awali walitengwa na jamii ya Israeli.
            1) Sasa ni Israeli ya kiroho.
                a) Rum.2:29; Gal.3:9,16.
        c. Awali walikuwa wageni wa maagano ya ahadi.
            1) Sasa wako chini ya Agano Jipya.
                a) Ebr.7:19; 8:13.
        d. Awali walikuwa hawana tumaini.
            1) Sasa Kristo ni tukufu wa tumaini lao.
                a) 1 Tim.1:2; Ebr.6:19,20.
        e. Awali walikuwa hawana Mungu duniani.
            1) Sasa wameufia ulimwengu, na kuwa hai katika Mungu.
                a) Rum.6:1-8.
    2. Limewezekana hili kupitia damu ya Kristo.
        a. Ebr.9:22; 10:4.
        b. 1 Pet.1:18,19.
        c. Ufu.1:5; Efe.1:17; Kol.1:14.

**Mstari wa 14,15 -** "*Kwa maana yeye ndiye amani yetu*."
    1. Isa.9:6; Efe.6:15; Flp.4:7; Yoh.14:27.

A. "*Aliyewafanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja*."

1. Efe.3:4-6; Rum.1:16; Gal.3:26-29.
    a. Hakuwaingiza Mataifa katika jamii ya Kiyahudi. Wala hakuwaingiza Wayahudi katika jamii ya Mataifa. Bali aliifanya jamii mpya, mwili mpya.
        1) Tofauti ya kale lazima itoweke kabisa sasa.

B. "*Akakibomoa kiambaza cha kati…ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo*."
1. Katika hili tunashughulikia Agano la Kale.
    a. Warumi sura 7 hubainisha tatizo alilokuwa nalo mwanadamu – sheria ilikuwa "takatifu, ya haki, na njema."

2. Agano la Kale liliondolewa kwa kuwa lilitekeleza kusudi lake.
    a. Gal.3:19-24.
        1) Mwa.22:18; Gal.3:16.
            a) Wayahudi, angalau mabaki, walihifadhiwa ili kutimiza kusudi lake.
            b) Lilimtambulisha kwetu Kristo ambaye ndiye atawahesabia haki wenye dhambi.
                (1) Ebr.10:1; Kol.1:27.

C. "*Ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake, akafanya amani*."
1. Baina ya Wayahudi na Mataifa.
    a. Gal.3:28.
    b. Warumi.
        1) 1:16.
        2) 2:9.
        3) 3:10; 3:23.

**Mistari ya 16-18** – <u>Kupatanishwa na msalaba</u>.
A. 2 Kor.5:17-21; Kol.1:21; Rum.5:10.

B. Upatanisho –
1. (KATALLASSO).
    a. Haswa likilenga kugeuka, kubadilisha (fedha); (watu) kutoa uadui hadi urafiki.

2. (APOKATALLASSO).
    a. Muundo wenye nguvu zaidi.
    b. Kubadilika kutoka hali moja hadi nyingine, ili kuondoa uadui wote na kutoacha kizuizi chochote kuelekea umoja na amani.

C. Msalaba.
1. Damu hutakasa na kutibu madoa ya dhambi.

D. Upatanisho huu ni kwa watu wote.

E. Kupitia Kristo Yesu.
1. Yoh.14:6; Mdo.4:12.

F. "*Katika roho mmoja*."
1. 1 Kor.12:13.
    a. Kazi za Roho katika wokovu.
        1) Mdo.2.
        2) Yoh.3.

**Mistari ya 19-22** – <u>Sasa hekalu lenye utukufu</u>.

A. 1 Pet.2:9.
   1. Sasa tumekuwa wageni kwa ulimwengu.
      a. Rum.6.

B. 1 Tim.3:15.

C. Msingi wa kanisa.
   1. 1 Kor.3:11.

## WAEFESO SURA YA TATU

**Mstari wa 1 -** "*Kwa sababu hiyo mimi Paulo ni mfungwa wake Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi Mataifa*."

A. "*Kwa sababu hiyo mimi Paulo*."
   1. Paulo amekwisha jadili nafasi muhimu jinsi Wayahudi na Mataifa walivyopatana na Mungu na kuwa mwili mmoja. Amebainisha jinsi wote wawili – Myahudi na Mmataifa, walivyopatanishwa katika Kristo na kufanya makazi ya Roho.

   2. Tambua, hadi kufikia mstari wa 14 Paulo ataendeleza wazo hili.
      a. Atachepuka na kujijadili yeye mwenyewe na ofisi yake kama mtume.
         1) Suala hili si la fedheha.
            a) Bado anajadili suala la neema iliyowafikia Mataifa, jambo alilolijadili kwa kina katika sura ya pili.
            b) Kwa kukazia agizo alilopewa Paulo, inaonyesha Mungu alivyowajali watu wa Mataifa kwa kiwango kikubwa.

B. "*Mfungwa wa Kristo*."
   1. Kumbuka, hii ni moja ya nyaraka zinazojulikana kama "Nyaraka za Gerezani."
      a. Wakili aliye katika minyororo – Efe.6:20.
      b. Kifungo cha injili – File.13.
      c. "Kwa maana nimefungwa kwa mnyororo huu kwa ajili ya tumaini la Israeli."
      d. "*Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu*."

   2. 1 Pet.4:12-16.
      a. Yoh.15:20,21.

C. "*Kwa ajili yenu Mataifa*."
   1. Nilifanywa kuwa mfungwa katika Rumi kwa ajili yenu, kwa kuwa nilishikilia kwamba injili ni lazima ihubiriwe kwenu ninyi Mataifa. (Angalia Mado.22:21-23. (Pia Barnes Notes, p. 984.)

   2. Paulo alitumwa haswa kwa Mataifa, Rum.11:13; Gal.2:9.
      a. Elewa mpangilio wa kitabu cha Matendo.
      b. Kadhalika tambua hili lilikuwa si sheria nzito na ngumu.

**Mstari wa 2 -** "*Ikiwa mmesikia habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu*."

A. "*Ikiwa mmesikia*."

1. Wuest anasema, "Ni tabia ambayo mara nyingi hatushukuru kama tupasavyo.
2. Alford anasema, "Waefeso walisikia mambo haya yote, na Mtakatifu Paulo sasa kwa maneno ya kuvutia akiwakumbusha."

B. "*Ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu*."
   1. Angalia Efe.1:9, 10.
   2. Tena jambo hili linaijadili mada. Paulo alitumwa kwa Mataifa, ambao walikuwa na haki katika wokovu wa Mungu sawasawa na Wayahudi.
      a. Rum.1:16; Gal.3:28; Mdo.10:34; rum.2:11.
      b. Kumbuka kusudi la kuandika kitabu.

**Mstari wa 3 -** "*Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache*."

A. "*Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo: (kama nilivyotangulia kuandika katika maneno machache*)."
   1. Utume wa Paulo hutegemea katika jambo hili.
      a. Mdo.26:16-18.
      b. Gal.1:11,12.

   2. Tambua sifa za mtume hupelekea kupokea ufunuo wa moja kwa moja.

B. "(Kama nilivyotangulia kusema kwa maneno machache.)"
   1. Watu wengi wanakubaliana kwamba Paulo anarejea nyuma katika mambo aliyotangulia kuangalia 1:9,10 na 2:18.
   2. Hata kama ni waraka mwingine haitupi shida yoyote sisi.
      a. 2 Pet.1:3; 2 Tim.3:16,17.

**Mstari wa 4 -** ("*Kwa hayo, myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo*."

A. ("Kwa hayo…Kristo.")
   1. "Mambo ambayo Paulo aliandika kuhusu kuitwa kwa Mataifa katika sura iliyotangulia ilikuwa ishara ya ufahamu wake katika mpango mzima wa wokovu, hapa imetajwa kama 'siri ya Kristo,' ambayo yanajumuisha ukweli wote kwamba Mataifa walikuwa 'washiriki' wa ahadi katika Kristo Yesu kupitia injili" (D. Lipscomb, p. 57).

   2. Tunasoma pia kwamba tunaweza kuelewa Biblia.
      a. Tutalijadili hili kwa kina hapo baadaye.

   3. Angalia notisi katika Efe.1:9.

**Mstari wa 5 -**"*Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho*."

A. "*Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine*."
   1. 1 Pet.1:10-12.
      a. Angalau, si katika namna ya kuthibitisha jinsi mtu anavyoumbwa kuwa mpya. Agano la Kale lilinena habari za watu wa Mataifa lakini Wayahudi walidhania wangelikwenda kwa njia ya ngazi ya Kiyahudi. Hili ndilo lilikuwa tatizo kubwa ambalo Wakristo karne ya kwanza walikabiliana nalo.

        1) Mdo.15:13-21.

B. “*Kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii …katika Roho*.”
   1. Tena, ni lazima tusisitize kuwa ni siri pale tu pasipokuwepo ufunuo.
   2. Pia Paulo hakuwa yeye pekee mwenye kupokea ufunuo.
      a. Mitume watakatifu na manabii kwa njia Roho walipokea ufunuo.
         1) Manabii – ni watu ambao walifanya kazi ya nabii au mwalimu aliyevuviwa katika kanisa changa.

**Mstari wa 6 -**“*Ya kwamba Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili*.”

A. “*Ya kwamba Mataifa …Kristo*.”
   1. Rum.2:25-29.
   2. Gal.3:9 na 16.
   3. Angalia kwamba maneno haya “katika Kristo” yametokea tena.

B. “*Kwa njia ya injili*.”
   1. Rum.1:16, 17; 2 Thes.2:14.
   2. 1 Kor.9:16; 1Thes.2:4.

**Mstari wa 7 -** “*Injili hiyo ambayo nilifanywa kuwa mhudumu, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake*.”

A. “*Injili hiyo ambayo nilifanywa kuwa mhudumu*.”
   1. Kuwa mhudumu ni nini?
      a. Nini maana ya neno ambalo Paulo analitumia?
         1) Inawezekana tukawa na hatia?

B. “*Kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa*.”
   1. Paulo alihesabu utumishi wake kama fursa kubwa aliyopewa kwa neema ya Mungu.
      a. 1 Thes.2:4.

   2. Katika mistari ya 2,7, na 8 Paulo anajadili jambo hili.

C. “*Kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake*.”
   1. Ni namna gani mtesi kugeuka kuwa askari muumini hodari katika kambi ya maadui?
      a. Halikukamilishwa na Paulo peke yake.
      b. Halikufanyika na mtu binafsi.
      c. Ilichukua injili hiyo hiyo ambayo iliwaingiza Mataifa mahali hapa.
         1) Md.20:24; Angalia mstari 2, 7 na 8.
         2) Rum.16; 2 Kor.10:4,5.

**Mstari wa 8 -** “*Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika*.”

A. “*Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote*.”
   1. Awali Paul aliliudhi kanisa.
      a. 1 Kor.15:9; 1 Tim.1:13.

2. Barnes anabainisha kwamba Paulo anaunda neno ambalo halijatumika popote katika Agano Jipya. [Angalia lugha – "mdogo kuliko yeye aliye mdogo'] (p. 985). "Kwa neema yake Mungu nimekuwa jinsi nilivyo."

3. Kumbuka maneno ya Matendo 9:4.

B. "*Nalipewa neema hii*."
   1. Tena, Paulo anatambua ni fursa kubwa kuhubiri injili kwa Mataifa.
      a. 1 Thes.2:4; 1 Kor.9:16.

C. "*Kuwahubiria Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika*."
   1. Usiopimika (ANEXICHNIASTOS) – usio na kifani.
      a. Linapatikana mahali pengine pamoja tu katika Agano Jipya.
         1) Rum.11:33. "Usiochunguzika."

   2. Wazo la kuwa na utajiri mwingi kwa watu wote ulimfanya kuona kazi yake kuwa ni muhimu sana, aliyeinuliwa juu sana kupita kiasi ambapo ulimwengu hudharau, akajawa na shukrani kwa Mungu kwa kutunukiwa juu yake (D. Lipscomb, p. 59).
      a. Hakika mhubiri wa kweli wa injili ana kazi iliyotukuka ya uwakili wenye utajiri upitao ufahamu.
         1) Kumbuka pia 1:18.

**Mstari wa9 -**"*Na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote*."

A. "*Na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo*."
   1. Watoa maoni wengi wanakubaliana kwamba "ushirika" linaweza kutafsiriwa "kipindi fulani."
      a. Ilikuwa fursa ya Paulo, kwa neema ya Mungu, "kuleta nuru" (PHOTIZO), siri.
      b. Katika kila hali, Kristo ni siri. Kitabu cha Wakolosai.
         1) Lakini hili linahitaji eneo pana. Angalia 1:9.

B. "*Ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu*."
   1. 1 Pet.1:10-12.
      a. "Mungu hawiwi na yeyote kueleza kwa nini jambo hilo lilifichwa kuwa siri kwa muda mrefu." (W.G. Blaikie, Pulpit Commentary, Vol.20, p. 106).

   2. Matendo 15:18.
      a. Kwa kadiri ya mpango wa ukombozi ulivyo ni lazima kuanzia mwanzoni mtu lazima arejee kabla ya Mwanzo 1:1.
      b. Jambo hili linakuwaje kwa mtazamo wa kanisa wa utawala wa Yesu wa miaka elfu duniani (premillenniaalists)?
         1) Watu wanaoamini utawala wa Yesu wa miaka elfu duniani wanamtumikia mungu duni ambaye yumo akilini mwao. Huyo si Mungu wa Biblia!

C. "Aliyeviumba vitu vyote katika Kristo Yesu."
   1. Kol.1:15,16; Yoh.1:1-4.
      a. Kwa nini Paulo aliijadili pointi hii hapa, ingawa ni rahisi kuielewa, nje huku ni swali linalofurahisha. Jambo hilo binafsi ninatarajia kulifanyia uchunguzi zaidi.
         1) Naweza kurudi nyuma katika haki ya Mungu ya kuificha siri na kuifunua wakati wake aliopenda.

a) “Kwa maneno haya imeonekana ukuu katika Mungu husimamia ukweli wa kwamba vitu vyote asili yake ni yeye, kwa sababu hiyo si tu anapanga mambo kulingana na mapenzi yake (1:5), bali pia nyakati za utimilifu kulingana na hekima yake isiyopimika inayoona kila namna inayofaa na bora, huteua mjumbe ambaye angetangaza ukweli wa ukuu wake anaotaka” (D. Lipscomb, p. 60).

**Mstari wa 10 -** “*Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho*.”

A. “Ili sasa, … na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho.”
  1. Kuna mitazamo mbalimbali kuhusu “falme na …ulimwengu wa roho.”
     a. John Locke: Serikali na wenye mamlaka katika ulimwengu wa roho ni viongozi wa dini wa Kiyahudi.
     b. MacKnight: Ni malaika katika ngazi mbalimbali mbinguni.
     c. Calvin, Hodge, Grosheide na Lenski walifikiria kwamba haya yanawalenga malaika wema mbinguni.
     d. A.T. Robertson alielewa rejea inalenga kwa “nguvu ya Ibilisi au malaika walianguka, pekee.”
        1) Yote haya yalitolewa kutoka katika Fafanuzi za Burton Coffman ukurasa wa 187.
     e. D. Lipscomb: Malaika katika ngazi mbalimbali (Uk. 60).
     f. Curtis Cates: Malaika watakatifu, ambao zamani waliinama chini wakijaribu kuangalia mpango wa ukombozi. (The ninth annual Spiritual Sword Lectureship Book on Ephesians, p. 67.
     g. Coffman: Ana maana ile ile kama alivyoandika: “Tutapaza sauti zetu kwa ujumbe wa injili kwake aliye juu sana mbinguni na kusifu utukufu wa kanisa kama ulivyodhihirika kama ufunuo wa hekima ya Mungu mbele ya viumbe vyake vilivyo juu sana ya ulimwengu” p. 187.

  2. Efe.6:12.
     a. Fungu hili linafurahisha kujifunza bila upendeleo. Fungu linalohitaji nguvu na muda wetu bila shaka.

B. “Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu…ijulikane.”
  1. Mitume walifanywa kuwa tamasha ya ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu (1 Kor.4:9).
  2. Angalia pia Ebr.12:22. “Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi.”
     a. Malaika wanajifunza kutokana na kuwepo kwa kanisa na baraka hekima za Mungu zaidi na zaidi.

C. “*Hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi*.”
  1. “Hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi” (POLUPOIKILOS), yaani “yenye rangi nyingi,” au “namna mbalimbali”tunawezalinganisha na kugawanya mawimbi ya mwanga (wenye rangi nyingi, kama ilivyo) kwa mtu kuupeleka mwanga kupitia katika tone la maji au mche (prism). Kanisa huifanya hekima ya Mungu bora iwe na nakshi isiyoelezeka kwa uzuri. Mtu anaweza kushukuru ugumu wa kuelewa mambo waliozoelea hawa viumbe watakatifu walipomtazama Mungu mtakatifu, asiyeweza hata kuangalia maovu (Ebr.1:13), akisamehe na kukaa na wanadamu waovu waliokuwa wakistahili mauti” (S.S.L., p. 67).
     a. Kuna maoni mengi mazuri kutokana na jambo hili:
        1) Neema na kifo cha Kristo (Ebr.2:9).
        2) Damu ya ukombozi (Ufu.1:5; Efe.1:7; Mdo.20:28).
        3) Kristo kufanyika kuhani mkuu na mwombezi (Ebr.2:17;4:14-16).

4) Kuwapatanisha Wayahudi na Mataifa (Efe.2:13-16; 3:6).
5) Bibi arusi (kanisa) na bwana arusi (Kristo) (Isa.62:5; Rum.7:4; Efe.5:23-31; Wimbo Ulio Bora).

**Mstari wa11 -** "*Kwa kadiri ya kusudi la milele alilokusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu*."

A. "Kwa kadiri ya kusudi la milele."
   1. Angalia notisi katika Efe.1:4.
   2. Tena tunaona kwamba hili si suala la Mungu kubadilisha mpango (a secondary plan).

B. "Alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu."
   1. Angalia jinsi Kristo alivyo wazo kuu tena. Kila unapojifunza kitabu chochote cha Biblia huwezi kusoma mahali bila kukutana na wazo linalomhusu Yesu. Yeye ndiye pointi kuu ya umilele.

**Mstari wa12** – "*Katika yeye tunao ujasiri na uwezo wa kukaribia katika tumaini kwa njia ya kumwamini*."

A. "Katika yeye…kumwamini."
   1. Katika Kristo, tumefanyika kuwa makuhani katika ufalme wa mbinguni (1 Pet.2:9; Ufu.1:6).
      a. Kupitia mpatanishi wetu (1 Tim.2:5), kwa ujasiri, au kwa lugha rahisi, tunakiendea kiti cha enzi cha neema.
         1) Ebr.4:16; pia angalia Ebr.10:19.

   2. Bali pia tutatambua ujasiri huu asili yake ni wapi.
      a. Hilo litasababisha kuwa na kicho na heshima.
         1) Isa.6:1-5; Eze.1:26-28.
         2) Ayubu 9:32.

**Mstari wa13** – "*Basi naomba msikate tamaa kwa sababu ya dhiki zangu kwa ajili yenu, zilizo utukufu kwenu*."

A. 2 Tim.1:8.
   1. Kumbuka ni kwa nini Paulo alifungwa.
      a. Hakutaka waongope kutokana na kufungwa kwake.
         1) Flp.1:14.

Katika mstari wa14 Paulo atarejea katika jambo ambalo alilianza awali kabla hajachepuka kuendelea na Myahudi na Mmataifa kufanyika mmoja katika Kristo na kupatanishwa na Mungu. Katika sala hii A.T. Robertson katika juzuu (volume) IV ya kitabu chake, *Word Pictures in the New Testament*, anasema, "Haswa kuna maombi aina tano katika sala hii kuu zaidi ya Paulo…hakuna mahali pengine ambapo Paulo anakizama ndani zaidi kihisia au kuwa juu kabisa kihisia au kiunuka kiwango fulani kwa huruma kiroho kama hapa. Mambo yote yanaonekana kuonekana kwa "wingi wa utajiri wa utukufu wake."" (p. 532).

**Mstari wa14** – "*Kwa hiyo nampigia Baba magoti*."

A. Kwa hiyo…Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo."
   1. Angalia notisi katika Efe.1:16.

**Mstari wa 15** – "*Ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa*."

A. "Ambaye….unaitwa."
    1. Lipscomb anaandika hivi, "Familia yote – watumishi, malaika, roho za wenye haki wanadamu zimefanywa kuwa kamilifu mbinguni, na Wakristo duniani ni familia moja iliyoitwa kutoka kichwa na Baba, Mungu, kama vile familia duniani huitwa jina lake kutoka kwa kichwa na baba wa familia" p. 62.

    2. Eerdman anabainisha ukweli kwamba Mungu ni Baba wa wote, katika hili yeye ni Muumbaji wa vitu vyote. Lakini, wazo hili lisichanganywe na maana maalum ya waumini kuwa "wana wa Mungu." Efe.5:1 na 1 Tim.3:15 ni katika mtazamo huu wa wana.
        a. Linatukumbusha wazo la "ndugu." Kwa maana moja wote ni ndugu, wakati maana nyingine ni waumini tu ambao ni ndugu na dada.

**Mstari wa 16** – "*Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani*."

A. "*Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake*."
    1. Ni kitu kinamfanya Mungu awe na utukufu?
        a. Je, si tabia yake kwa ujumla inayomfanya Mungu atukuke?
        b. Katika sura zilizotangulia, tumelijadili hili la "utajiri." Hapa inalenga kujaa tele.

    2. Basi ni kulingana na vyote vinavyomfanya Mungu kutukuka.

B. "*Kufanywa imara kwa nguvu*."
    1. Angalia notisi katika Efe.1:1.
    2. Paulo anatamani watiwe nguvu ili kwamba watimize majukumu yao mbalimbali. Kama Barnes anavyosema, "kuwapeni nguvu nyingi ili kuyastahimili majaribu (trials), kuyapinga majaribu (temptation), kutekeleza wajibu wake, kuishi maisha ya imani" p. 987. D. Lipscomb anabainisha pia katika maoni yake juu ya suala hili.

C. "*Kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani*."
    1. Kiini cha nguvu – Roho Mtakatifu.
        a. Kumbuka Efe.2:21,22.
            1) Mdo.2:38,39; Efe.1:13; 1 Kor.6:19,20.
            2) Rum.8:31; Flp.19.
                a) Naam, hili hutegemea uhusiano wetu na Mungu.

    2. Utu wa ndani ndio unaomfanya mtu haswa.
        a. Huona hali maisha halisi (Zab.119:18.
        b. Rum.2:28,29; 2 Kor.4:16; 1 Pet.3:4.

    3. Utu wa ndani unatakiwa kuimarishwa kwa nguvu na Roho yake.
        a. Sasa mwanadamu ana sehemu katika hili. Haliwezi kukamilika bila ya mwanadamu.
            1) Angalia Efe.6:10,11.
            2) Flp.2:12,13.

    4. Ni jinsi gani Roho hufanya haya?
        a. Kol.1:9-11.
            1) Angalia Paulo anavyokazia kuhusu maarifa (knowledge).
            2) Pia angalia Zab.19:7-11.

b. 2 Tim.3:16,17; 2 Pet.1:3.
c. Efe.4:7-16.
d. Msimamo wa utendaji.
    1) Kuyashinda majaribu.
        a) Math.4:4,7,10.
        b) Zab.119:9-11.

    2) Ni jinsi gani juu ya wajibu wangu?
        a) Maandiko yananifundisha kuchukuliana na ndugu pamoja na mahitaji yake.
            (1) Gal.6:2.

        b) Kwa kujizatiti katika kutenda mapenzi ya Mungu (Yak.1:22), je najitoa mwenyewe kama chombo chenye kufaa kwa Mungu?
            (1) Je, sipo mimi mahali pa kutumiwa kimajaliwa?
                (a) Ni kitu gani kinaweza kunisaidia kunirejeza?
                    [1] Neno la Mungu.

**Mstari wa 17** – "*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo*."

A. "*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani*."
    1. Angalia notisi katika Efe.2:22.
        a. Mungu awali alikaa hekaluni, sasa anakaa kanisani.

    2. Lipscomb analenga kwa Wakolosai 1:9-11 kama wazo moja katika maneno mengine.
        a. Lakini hili si tofauti na neno la Mungu.
            1) Rum.10:17; Yoh.20:30,31.
            2) Kol.3:16.

B. "*Mkiwa na shina na msingi katika upendo*."
    1. Shina – kama mti uimara wake ni katika mfumo wa mizizi yake.
    2. Msingi – kama jengo lilivyo imara kutokana na msingi wake.
        a. Math.7:24-27.
        b. Wanapaswa kuimarika katika upendo mithili ya mti katika udongo kwa sababu ya mizizi yake kwenda chini au jengo lilivyo juu ya msingi imara.
    3. Upendo eneo lake ni pana sana.
        a. Mk.12:30,31.
        b. 1 Pet.2:17.
        c. Math.5:44.

**Mstari wa 18** – "*Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo na kina*."

A. "*Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu*."
    1. Paulo alitaka watambue.
        a. Kumbuka Efe.1:18,19.
        b.Lakini, kuna tabia ambazo unapaswa kuwa nazo.
            1) Math.5:8; 6:22; Yoh.7:17.

B. "*Jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo na kina*."
    1. Upana.

        a. Huwafikia watu wote (Ebr.2:9), na ni bure mfano wa hewa tunayoivuta.
            1) Lk.4:18 panatoa wazo la upana.

        b. Sio tu kwa rafiki zake, bali pia kwa adui zake.

    2. Urefu.
        a. Yoh.13:1; 15:13,15.
        b. Wakati wote upendo wa Bwana ulipoanza kutenda kazi haukupungua kamwe hadi aliposema, “imekwisha.”

    3. Kina.
        a. Unashuka chini kiwango gani?
            1) 1 Tim.1:15; Efe.2:1-3; Mdo.2 na hotuba ya Petro.
                a) Hakika katika hili tunaweza kupata dhana ya kina cha upendo wa Kristo.

    4. Kimo.
        a. Kristo aliyetukuka anapenda sisi kushiriki kuona hili.
            1) Yoh.17:24; Rum.8:17; 2 Tim.2:12.

**Mstari wa 19** – “*Na kuujua upendo wake Kristo upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu*.”

A. “*Na kuujua upendo wa Kristo*.”
    1. Rum.5:8; Yoh.15:13; Ufu.1:5.
    2. “Hakuna kitakachochochea shukrani mioyoni mwetu; hakuna kitu kinachotusukuma kujikana wenyewe; hakuna kitakachotufanya tuwe wakarimu na hatimaye kuwa wafu kwa ulimwengu ni upendo wa Kristo” (Barnes, p.987).

B. “*Upitao ufahamu*.”
    1. Utofauti wa upendo wake unapita ufahamu wetu.
        a. Rum.5:7.
        b. Rum.5:8.
        c. 2 Kor.8:9.

C. “*Mpate kutimilia kwa utimilifu wote wa Mungu*.”
    1. Jambo hili lisichukuliwe katika fungu la maneno (phrase) lililotangulia, bali kutoka katika sentensi nzima.
        a. Efe.4:13; 2 Kor.3:18; 1 Yoh.3:2; Flp.3:20,21.

**Mstari wa 20** – “*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu*.”

A. “*Basi…yeye*.”
    1. Si jambo la ajabu kwa Paulo kuzama katika mawazo ya kusifu anapozumzia baraka nyingi ambazo Mungu alizishusha kwetu.
        a. Gal.1:5; Rum.9:5; Rum.11:36.

B. “*Awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo*.”
    1. “Katika kumzungumzia Mungu ni kama kufikiria nafasi ambayo hata hivyo ni mbali na mawazo yetu tunapoweza kwenda nje na uwezo wetu. Paulo alikuwa ameomba mno katika sala hii, na

mawazo yanaweza daima kufika mbali na maneno, lakini uweza wa Mungu umezidi upeo wote. Uweza wa Mungu umetajwa katika maneno mawili yenye kuonyesha kuzidi (exceedingi abundantly), kama vile mtume anavyotarajia mioyo yetu kujawa na wingi wa uweza wa neema yake Mungu" (D. Lipscomb, p. 68).

2. "Hii ni namna moja Paulo akionyesha uwezo mkubwa mno, akiweka bayana uweza wa Mungu wa kutujalia yote tumwombayo na kufikiria" (F.F. Bruce, The Epistle to the Ephesians, p. 70).
    a. 1 Thes.3:10.
    b. 1 Kor.2:9.

C. "*Kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu*."
    1. Angalia notisi katika 1:19,20.

**Mstari wa 21** – "*Naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele*. *Amina*."

A. "*Naam, atukuzwe katika Kanisa*."
    1. Hapa tunaona kusudi la kanisa.
        a. KUMTUKUZA MUNGU.
            1) Tunafanyeje hivi?

    2. Rum.16:27.

B. "*Na katika Kristo Yesu*."
    1. Hakuna mahali pawili ambapo mtu anatakiwa kumtukuza Mungu.
        a. "Katika kanisa" na "katika Kristo", na "katika Kristo Yesu" kama tafsiri nyingine zilivyotafsiri (NIV) ni jambo moja linaloongelewa.
            1) Huwezi kumtukuza Mungu nje na kanisa. Haiwezekani kabisa.
            2) Yoh.15:1-8; 2 Pet.1:5-10.

C. "*Hata vizazi vyote vya milele na milele. Amen*."
    1. "Yaani ni hivi haswa, 'kwa vizazi vyote miaka hata miaka,' au 'kwa vizazi vyote vya milele hata milele (eternity of eternities), au milele kwa miaka yote.' Ni lugha ya kuonyesha upendo TELE wa Mungu, na akipendezewa kwamba angesifiwa pasipo kikomo milele na milele" (Barnes Notes, p. 988).
        a. Zab.72:17; 45:17; Ufu.5:13.

## WAEFESO SURA YA NNE

**Mstari wa 1**

A. Wito wetu.
    1. 2 Thes.2:14.
    2. Yak.2:7 – "…jina lile zuri mliloitiwa."
        a. 1 Pet.2:9 – Tumeitwa toka gizani.
        b. 1 Pet.2:21 – Tumeitwa tufuate nyayo za Kristo.
        c. 1 Pet.3:9 – Tumeitwa tuyashinde mabaya kwa kutenda mema.
        d. 1 Pet.5:10 – Mungu ameita katika utukufu wake wa milele.
        e. Yuda 1 – Tumetakaswa na kuhifadhiwa na kuitwa.

B. Tuenende kama inavyostahili wito wetu.

1. Palipo baraka kuu basi majukumu yake ni makubwa pia.
    a. Rum.12:1,2; 2:4.
    b. Efe.4:1-6 tutajadili umoja. Kuna pointi nne ambazo tungependa zijadiliwe chini ya mada hii.

**Mstari wa 2**

A. Jinsi (attitudes) ya umoja.
  1. Unyenyekevu (TAPEINOPHROSUNES).
  2. Upole (PRAUTETOS).
  3. Uvumilivu (MARROTHUMIAS).
  4. Mkichukuliana katika upendo (ANECHOMENIO) – kuinuana, kuvumiliana, kustahili.

B. Upendo ni kiungo muhimu.
  1. Kol.2:2.
  2. Rum.12:10.
  3. Yoh.13:35.
  4. 1 Pet.1:22.
  5. 1 Pet.2:17.

**Mstari wa 3**

A. Msimamo wa umoja.

B. Jinsi ya kutambua umuhimu wa watu kuwa wamoja.
  1. Efe.4:4; 1 Kor.12:20; Kol.1:18; Efe.1:22,23.
  2. Math.16:13-18.
  3. 1 Kor.1:10-13.
  4. Flp.2:2.
  5. Zab.133:1; 34:3.
  6. Yoh.17:20,21.

**Mstari wa 4-6**

A. Ulingo (platform) wa umoja.
  1. Mwili.
      a. 1 Kor.12:20.
      b. 1:18; Efe.1:22,23.
      c. Yoh.15.
      d. Namna gani Rum.16:16?

  2. Roho.
      a. Roho Mtakatifu
          1) Mungu.
          a) Mdo.5:3,4.
          b) Mdo.5:32.

  3. Tumaini la wito wenu.
      a. 1 Tim.1:1; Ebr.6:19,20.
      b. Rum.8:24.
          1) 1 Pet.1:3.
              a) Ufufuo.

  4. Bwana.

a. Yesu Kristo.
    1) Ufu.17:14.

5. Imani.
    a. Yuda 3.
    b. Mdo.6:7.
    c. Gal.1:23.
        1) Mafundisho au mwili wa mafundisho ambayo hatimaye tumepata kutoka kwa Mungu.

6. Ubatizo.
    a. Ubatizo mbalimbali.
        1) Yohana Mbatizaji.
        2) Ubatizo wa Roho Mtakatifu.
        3) Ubatizo wa mateso.
        4) Ubatizo wa moto.
        5) Ubatizo wa wafu.
        6) Ubatizo unaohusiana na Agano la Kale.
        7) Ubatizo wa Agizo Kuu.

